JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

# MAARIFA YAJAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

## 614 MAARIFA YAJAMII

*Kimechapwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI....................................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI .......................................................................................... 1
2.0 TATHIMNI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI........ 3
2.1 Tathmini A: Maswali ya Majibu Mafupi .......................................................... 3
2.1.1 Swali la 1: Nchi Yetu Tanzania ............................................................. 3
2.1.2 Swali la 2: Sayari Dunia............................................................................ 6
2.1.3 Swali la 3. Sayari Dunia.......................................................................... 10
2.1.4 Swali la 4. Sayari Dunia.......................................................................... 12
2.1.5 Swali la 5. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani............................. 15
2.1.6 Swali la 6. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika ......................................................................... 18
2.1.7 Swali la 7: Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira. .......................................................................................... 21
2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii baada ya Afrika Huru ............................................................................................. 25
2.1.9 Swali la 9: Mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii Baada ya Afrika Huru ............................................................................................. 28
2.1.10 Swali la 10: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni .......................... 31
2.2 Tathmini B: Maswali ya Insha........................................................................ 34
2.2.1 Swali la.11: Nchi Yetu Tanzania .......................................................... 34
2.2.2 Swali la: 12. Sayari Dunia....................................................................... 39
2.2.3 Swali la 13: Ushirikiano wa Kimataifa ................................................... 44
2.2.4 Swali la 14: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni .......................... 51
2.2.5 Swali la 15: Upimaji na Tathmini ........................................................ 56
2.2.6 Swali la.16. Ufundishaji wa Mada za Historia...................................... 61
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA66
4.0 HITIMISHO........................................................................................... 67
5.0 MAPENDEKEZO.................................................................................... 68
KIAMBATISHO........................................................................................... 69

# DIBAJI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Ualimu Daraja A uliofanyika Mei 2021 kwa masomo ya Jiografia na Histroria. Masomo ya haya hutahiniwa kwa pamoja katika mtihani wa Maarifa ya Jamii. Lengo la kuandaa tarifa hii ni kutoa mrejesho kwa, watunga sera, wakufunzi, walimu tarajali na wadau wengine wa elimu. Mitihani ni namna mojawapo ya kufanya tathmini ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Tathmini hii inawezesha kubainisha ufanisi, changamoto pamoja na kutoa mapednekezo kuhusu mwelekeo wa namna bora ya kutekeleza mtaala wa ngazi husika.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada unaonesha kuwa, kati ya mada 10 zilizotahiniwa, ufaulu ulikuwa mzuri katika mada tano, wa wastani katika mada nne na hafifu katika mada moja. ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu uliofanyika umebaini kuwa, kwa ujumla, ufaulu katika mtihani huo ulikuwa mzuri kwani asilimia 99.83 ya watahiniwa walifaulu. Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, sababu za watahiniwa kutofaulu kwa kiwango kizuri zilikuwa ni pamoja na watahiniwa kutozingatia matakwa katika baadhi ya maswali, kuchanganya dhana na hivyo kutoa majibu ambayo hayakukusudiwa na watahiniwa, na kushindwa kutetea hoja zao kwa kuzingatia matakwa ya maswali husika. Uchambuzi wa kina na sababu za ufaulu katika kila swali umebainishwa.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, uchambuzi uliobainishwa kwenye taarifa hii utasaidia katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia; kwa kuzingatia hoja zilizotolewa kuhusu namna bora ya kujibu maswali pamoja ha dosari zilizobainishwa ambazo zinasababisha watahiniwa kuwa na ufaulu hafifu. Uchambuzi huu utawasaidia wakufunzi pamoja na walimu tarajali kufanyia kazi dosari zilizobainika na kuendeleza namna bora ya ufundishaji na ujifunza na hivyo kuwa na walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii katika shule za msingi. Baraza linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika maandalizi ya taarifa hii.

**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa mtihani wa Maarifa ya Jamii uliofanyika mwezi Mei 2021. Maswali ya mtihani yalitungwa kwa kuzingatia Mihtasari ya mwaka 2009 ya Ualimu Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ya masomo ya Jiografia na fomati ya Mtihani wa Maarifa ya Jamii ya mwaka 2017.

Mtihani wa Maarifa ya Jamii uligawanyika katika sehemu tatu A, B na C; zenye jumla ya maswali kumi na sita. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi ya majibu mafupi. Maswali matano yalitoka katika mada za somo la Jiografia na maswali matano mengine yalitoka katika mada za somo la Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu hii. Kila swali lilikuwa na alama nne hivyo kufanya jumla ya alama 40 katika sehemu hiyo. Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha. Sehemu hiyo iligawanyika katika vipengele viwili. Kipengele cha kwanza kilikuwa na maswali mawili yaliyotoka kwenye mada za taaluma za somo la Jiografia, na kipengele cha pili kilikuwa cha maswali mawili yaliyotoka katika mada za taaluma za somo la Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja kutoka katika kila kipengele. Kila swali katika sehemu hiyo lilikuwa na alama 15 hivyo, kufanya jumla ya alama 30 kwa maswali yote mawili ambayo mtahiniwa alitakiwa kujibu. Sehemu C ilikuwa na maswali mawili ya insha yaliyohusu ufundishaji. Katika sehemu hiyo, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo kufanya jumla ya alama 30. Kwa hiyo, katika mtihani wa Maarifa ya Jamii, mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne.

Uchambuzi kuhusu ufaulu wa jumla katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 2,983 walisajiliwa kufanya mtihani huo. Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 2,914 sawa na asilimia 99.83 walifaulu mtihani huo. Watahiniwa watano sawa na asilimia 0.17 Walipata daraja F. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umeshuka kwa asilimia 0.14 ikilinganishwa na ufaulu wa watahiniwa katika somo hilo mwaka 2020 ambapo watahiniwa wote (100%) walifaulu.

Katika kufanya uchambuzi, ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika makundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa asilimia za ufaulu katika makundi hayo ni 0 – 39, 40 – 69 na 70 – 100 mtawalia.  Sababu za watahiniwa kuwa na ufaulu hafifu, wastani au mzuri zimebainishwa. Ili kufafanua hoja zilizotolewa

kuelezea sababu za majibu ya watahiniwa, sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo ili kuonesha namna watahiniwa walivyoweza au kushindwa kujibu swali lililochambuliwa.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi utatoa mwanga kuhusu ufanisi na changamoto zinazohusu ufundishaji na ujifunzaji. Hii itawezesha wadau mbalimbali kuchukua hatua zinazolenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Historia na Jiografia.


## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 Tathmini A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali mafupi. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii. Hivyo, watahinwa wote 2,948 walifanya maswali hayo. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama 4. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika makundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa alama 0 - 1.5, 2 - 2.5 na 3 - 4 mtawalia.

#### 2.1.1 Swali la 1: Nchi Yetu Tanzania

Swali la kwanza lilitoka katika mada ya nchi yetu Tanzania. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kubainisha kwa kifupi aina nne za taka na vyanzo vyake. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa ulionesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani; kwani asilimia 67.3 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*


Kama Chati Na 1 inavyoonesha, asilimia 41.2 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walifaulu vizuri kwa kupata alama 3 hadi 4. Asilimia 26.1 ya watahiniwa wengine walikuwa na ufaulu wa wastani

wa alama 2 hadi 2.5 na asilimia 32.7 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa mahiri katika kutambua aina za taka na vyanzo vyake. Watahiniwa hao waliweza kuainisha taka mbalimbali na kubainisha vyanzo vyake kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kubainisha aina za taka kama *vile, taka ngumu, taka laini, maji taka* na *hewa chafu*. Watahiniwa hao pia waliweza kubainisha vyanzo vya taka hizo kama vile, *viwanda na shughuli za kibinadamu* ambazo huzalisha taka ngumu. Shughuli hizo ni kama vile vyuma chakavu, makopo, chupa tupu na vifaa vya plastiki.

Watahiniwa pia waliweza kubainisha vyanzo vya taka laini ambazo hutokana na mchanganyiko wa taka ngumu na vimiminika ambavyo vyanzo vyake ni viwanda na shughuli za kibinadamu kama vile masoko, taka kutoka kwenye makazi na mabaki ya vifaa vya kilimo. Aidha, watahiniwa waliweza kubainisha vyanzo vya uchafuzi wa hewa. Vyanzo hivyo, ni pamoja na *matumizi ya nishati ya mafuta* ambayo hutoa hewa chafu na *uchomaji wa vitu* mbalimbali ambao husababisha utoaji wa hewa ya ukaa ambayo huchafua hewa.


Kwa upande mwingine, watahiniwa hao waliweza kueleza vyanzo vya taka za vimiminika kama vile utiririshaji wa maji machafu ovyo, uchimbaji wa madini usiozingatia taratibu. Hali hii husababisha kemikali kuingia kwenye vyanzo vya maji na kuchafua pamoja na utiririshaji wa maji taka kutoka viwandani na kwenye makazi ya watu. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha aina za taka, na kuweza kueleza kwa kifupi vyanzo vyake.


1
(i) Taka ngumu:
hizi ni taka ambazo haziwezi kuoza mfano makopo ya maji hutokana na matumizi mbalimbali ya bidhaa
(ii) Taka Laini:
Hizi ni taka ambazo zipo kwenye mfumo wa yabisi na zinaweza kuoza chanzo ni kama vyakula
(iii) Taka za maji
hizi ni taka ambazo hutokea baada ya matumizi ya maji chanzo ni viwanda
(iv) Taka za hewa/gesi
hizi ni taka ambazo hutokana na hewa kuchafuka chanzo ni vyombo vya usafiri.

Kielelezo Na. 1: *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.*

Kwa kupande wa asilimia 26.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliweza kujibu swali hilo isipokuwa walikuwa na dosari kadhaa katika majibu yao. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja chache kuliko zilizokuwa zinahitajika. Watahiniwa wengine waliweza kutoa hoja zote nne ingawa baadhi yake hazikuwa sahihi hivyo kutopata alama zote. Majibu ya watahiniwa katika kundi hilo yalionesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za taka na vyanzo vyake.

Asilimia 32.7 ya waatahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili inaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za taka. Baadhi yao waliweza kuainaisha aina moja ya taka bila kuelezea au kutaja mifano ya aina mojawapo ya taka na kuviainisha kama aina nne tofauti. Kwa mfano, katika skripti ya mtahiniwa mmoja, aliandika *mkojo*, na *jasho* kama aina tofauti za taka ingawa kimsingi zote ni aina ya taka ya vimiminika. Mtahiniwa mwingine aliandika kama ifuatavyo; *(i) Taka za kemikali kutoka viwandani, (ii) taka za majumbani, (iii) taka za plastiki, (iv) taka zisizooza.* Katika majibu yake mtahiniwa alishindwa kuzitambua taka katika aina zake. Taka za majumbani kwa mfano zinaweza kuwa katika aina ya taka ngumu, taka vimiminika au taka laini kutegemea uzalishaji wake. Kielelezo Na. 2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na ufaulu hafifu katika swali hili.




1. i) Taka za plastiki
ii) Taka za viwandani
iii) Taka za mabaki ya Chakula
iv) Taka za kemikali

Kielelezo Na. 2: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1*

Katika Kielelezo Na. 2 mtahiniwa aliandika mifano ya taka badala ya aina za taka. Kwa mfano, taka za plastiki ni mfano wa taka ngumu na taka za kemikali zinaweza kuwa katika hali ya taka za aina za vimiminika, taka ngumu au taka hewa kutegemea aina ya kemikali. Aidha, jibu "taka za viwandani" lilikuwa la jumla mno kwani, taka hizo zinaweza kuwa taka ngumu, taka laini, taka vimiminika au uchafuzi wa hewa. Majibu ya mtahiniwa yanaonesha alikuwa na uelewa mdogo kuhusu taka lakini hakuweza kuzichambua katika aina zake.

### 2.1.2 Swali la 2: Sayari Dunia

Swali la pili lilitoka katika mada ya Sayari Dunia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi tofauti kati ya majanga ya asili na majanga ya kibinadamu. Takwimu zinaonesha kuwa, ufaulu katika swali hilo ulikuwa hafifu kwani ni asimia 20.3 tu ya watahiniwa ndio waliokuwa na ufaulu wa alama 2 hadi 4 ambao ni ufaulu wa wastani hadi mzuri. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa muhtasari.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*


Kama takwimu zinavyoonesha katika Chati Na. 2, asilimia 79.7 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5. Asilimia 11.5 ya watahiniwa wengine walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5, na asilimia 8.8 ya watahiniwa hao ndio waliokuwa na ufaulu mzuri wa alama 3.0 hadi 4.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulifanyika ili kubaini sababu za ufaulu wa watahiniwa katika kila kundi. Watahiniwa asilimia 79.7 waliokuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa walishindwa kutofautisha majanga ya asili na majanga ya kibinadamu. Wengi wa watahiniwa hao walitumia kigezo kimoja tu cha tofauti kati ya majanga ya asili na majanga ya kibinadamu yaani majanga ya asili kutokea kutokana na nguvu za asili na majanga ya kibinadamu kutokea kutokana na shughuli za kibinadamu. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa wengi kwenye kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti hizo za majanga. Katika kueleza tofauti hizo, watahiniwa walipambanua dhana moja wakiielezea kama dhana mbili tofauti jambo lililosababisha kupata alama za chini. Wengi wao walielezea majanga ya asili kwa maneno tofauti wakidhani walikuwa wakielezea majanga mawili tofauti. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo;

*Majanga ya asili ni majanga yanayosababisha vifo. Majanga hayo ni vimbunga, mafuriko, nguvu za volkano, tsunami, ukame. Lakini majanga yasiyo ya asili ni majanga ambayo pia husababisha kifo. Mfano ni tetemeko la ardhi, ukame, ajali ya moto n.k.*

Katika majibu yake, mtahiniwa hakutoa tofauti yoyote ya majanga hayo zaidi ya kutoa mifano ambayo hata hivyo, yote inahusu majanga ya asili.

Aidha, uchambuzi ulibaini kuwa watahiniwa hawakuwa na dhana sahihi kuhusu majanga. Kwani ili tukio lionekane kuwa ni janga ni lazima lihusishe uharibifu wa mali za watu na vifo. Pia tukio hilo litokee katika hali ya kushtukiza na litokee kwenye eneo wanaloishi binadamu. Hata hivyo, watahiniwa katika kundi hili walielezea matukio ya kijiografia kama vile mmomonyoko wa udongo. Walielezea pia shughuli za kibinadamu kama vile, ukataji wa miti ovyo na uchimbaji madini, kama mifano ya majanga ya kibinadamu hali iliyoonesha ukosefu wa maarifa kuhusu majanga. Kielelezo Na. 3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi katika kundi hili.


2. Majanga ya asili ni majanga yanayo sabab-
ishwa na nguvu asilia zilizomo ndani ya
ganda la dunia. Mfano Tetemeko la ardhi,
mripuko wa volkano, Tufani na Tsunami
WAKATI Majanga ya kibinadamu ni
majanga yanayotokea kutokana na shughuli
za kibinadamu Mfano wa majanga ya
kibinadamu ni ukame, mabadiliko ya hali
ya hewa na kutokea kwa jangwa.

Kielelezo Na. 3: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.*

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na dosari zilizowafanya wapate alama pungufu kuliko alama zilizoainishwa kwenye mwongozo wa usahihishaji. Katika kundi hilo, baadhi ya watahiniwa walirudia hoja kwa maneno tofauti na kuziwasilisha kama hoja tofauti na wengine walitoa ufafanuzi ambao haukujitosheleza. Watahiniwa wengine walitoa hoja pungufu kuliko zilizokuwa zinatakiwa ili kupata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

*Majanga ya asili*

*(i) Ukame – hutokea pale jua linapowaka sana na kusababisha mimea kukauka.*

*(ii) Mafuriko – hutokea kunyesha kwa mvua muda mrefu bila kuacha hivyo kupelekea mafuriko.*

*Majanga ya kibinadamu*


*(i) Kukata miti ovyo – Hii hutokea kukata miti bila kupanda miti inapelekea kukosa mvua ya kutosha.*

*(ii) Kutupa taka kwenye vyanzo vya maji.*


Mtahiniwa katika majibu yake alitumia mifano ya majanga kama hoja nne tofauti. Katika kuelezea majanga ya asili, mtahiniwa alitoa mifano miwili na siyo hoja mbili. Vile vile, katika kuelezea majanga ya kibinadamu, mtahiniwa alitoa mifano miwili ya majanga ya kibinadamu kama hoja mbili, ingawa hazikuwa sahihi.

Asilimia 8.8 ya watahiniwa waliojibu vizuri walibainika kuwa na maarifa yaliyotarajiwa kuhusu majanga ya asili na majanga ya kibinadamu. Vilevile walitofautisha majanga ya asili na majanga ya kibinadamu kwa ufasaha. Watahiniwa hao waliweza kutofautisha aina hizo mbili za majanga kwa kubainisha *tofauti ya vyanzo vya majanga hayo*. Watahiniwa walibainisha kuwa, *majanga ya asili husababishwa na nguvu za asili za dunia kama vile, nguvu kinzani aridhini ambazo husababisha matetemeko ya aridhi na vimbunga ambavyo husababishwa na upepo mkali unaoambatana na mvua nyingi ambazo husababisha mafuriko.*

Watahiniwa walibainisha zaidi kuwa ma*janga ya kibinadamu husababishwa na mahusiano kati ya binadamu kama vile vita na machafuko ya kisiasa*. Watahiniwa pia walitofautisha majanga hayo kutokana na uwezo wake wa kuharibu ndani ya muda mfupi. Waliweza kubainisha kuwa, *uharibifu unaotokana na majanga ya asili hutokea ndani ya muda mfupi ikilinganishwa na majanga ya kibinadamu*. Watahiniwa pia waliweza kubainisha kuwa *majanga ya kibinadamu yanaweza kuzuilika, lakini ni vigumu kuzuia majanga ya kiasili.* Aidh, watahiniwa waliweza kutofautisha majanga, hayo kwa namna yanavyoweza kutabirika. Ingawa kuna maendeleo ya sayansi ya teknolojia inayowezesha kutabiri majanga bado ni *vigumu kutabiri baadhi ya majanga ya kiasili kama vile tetemeko isipokuwa ni rahisi kuona viashiria vya majanga ya kibinadamu na kuchukua hatua.* Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa ambaye aliweza kutofautisha majanga hayo, licha ya dosari ndogo katika tahajia katika baadhi ya maneno.


2. (i) Majanga ya asili husababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa au hutokana na mazingira mfano tetemeko la ardhi wakati majanga ya kibinadamu hutokana na shughuli za kibinadamu mfano mlipuko wa mabomu.

(ii) Majanga ya asili ni vigumu kuyazuia wakati majanga ya binadamu yanaweza kuzurika kiurahisi.




(iii) Majanga ya asili yalikuwepo kabla ya binadamu kuwepo wakati majanga ya kibinadamu yametokea baada ya kuwepo kwa binadamu.

(iv) Majanga ya asili si ya kukusudia wakati majanga ya kibinadamu yanaweza kukusudiwa.

Kielelezo Na. 3. Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2

### 2.1.3 Swali la 3. Sayari Dunia

Swali la 3 lilitungwa kutoka katika mada ya Sayari Dunia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuainisha angalau vitu vinne vinavyounda mfumo wa jua. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 68.5 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama unavyooneshwa kwenye Chati Na. 2.





**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Takwimu katika Chati Na. 2 zinaonesha kuwa asilimia 42.0 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, Asilimia 26.5 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5 na asilimi 31.5 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 42.0 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo waliweza

kuainisha vitu vinne vilivyopo kwenye mfumo wa jua. Watahiniwa hao waliweza kuainisha vitu kama vile Jua, Sayari, satelaiti, vimondo/mateoridi na asteroidi. Majibu ya watahiniwa hao yalionesha kuwa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu vitu vinavyounda mfumo wa jua hivyo waliweza kupata alama za juu. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuainisha vitu vinne vinavyounda mfumo wa jua.



3. i/Sayari
ii) Kometi
iii) Asteroidi
iv) Jua

Kielelezo Na.4: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa jua. Baadhi ya watahiniwa hao waliorodhesha mchanganyiko wa baadhi ya vitu vilivyopo ndani ya anga la dunia na vitu vinavyounda mfumo wa jua hivyo kutopata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *mawingu, mwezi jua* na *nyota* kuwa ni vitu vinavyounda mfumo wa jua. Kati ya vitu hivyo, Jua na Mwezi ndiyo yalikuwa majibu sahihi japo Mwezi ni mfano wa satelaiti (jina la jumla kwa satelaiti za asili zinazozunguka sayari mbalimbali). Mawingu halikuwa jibu sahihi kwa kuwa mawingu ni sehemu ya sayari Dunia. Aidha, mtahiniwa huyo hakuwa na ufahamu kuwa Jua ni nyota ambayo ina mfumo wake wa sayari, satelaiti, vimondo na asteroidi na kwamba mfumo huo hauhusishi nyota nyingine. Mtahiniwa mwingine aliandika *sayari* na *vimondo* ambayo ni majibu sahihi na kushindwa kubainisha vitu vingine viwili.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walibainika kutokuwa na ufahamu kuhusu mfumo wa jua kutokana na majibu yao kutokuwa sahihi. Katika kundi hilo, baadhi ya watahiniwa waliorodhesha vitu vinavyoonekana katika anga la dunia kama vile mawingu, mionzi ya jua, mwanga na hali ya hewa. Kwa mfano, katika kujibu swali hilo, mtahiniwa mmoja aliandika vitu ambavyo havina uhusiano na mfumo wa jua ambavyo ni; *(i) Nguvu ya nishati (mwanga), (ii) Rangi (unapotumia kioo kutazama unaziona) (iii) Mionzi (inayosambaa baada ya jua kuwaka) (iv) Nguvu (chaji)*

Mtahiniwa mwingine aliainisha *nyota, mwezi na radi* kuwa ni vitu vilivyopo kwenye mfumo wa Jua. Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa hawakuwa na ufahamu wa mfumo wa Jua jambo lililosababisha ufaulu hafifu kwenye swali hilo. Kielelzo Na. 5 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.



3. i) Miale ya mwanga.
ii) Mzunguko wa dunia
iii) Mawingu
iv) Mabadiliko ya dunia kama kupatwa kwa mwezi.

Kielelezo Na.5: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3

Majibu ya mtahiniwa katika kielelezo Na. 5 siyo sahihi kwa kuwa, badala ya mtahiniwa kutoa vitu vilivyopo kwenye mfumo wa Jua, ameorodhesha vitu vinavyoonekana kwenye anga la sayari Dunia kama vile, mawingu na mieale ya Jua pamoja na matukio yanayoweza kutokea duniani kama kupatwa kwa Juna na Mwezi.

### 2.1.4 Swali la 4. Sayari Dunia

Swali la nne lilitungwa kutoka katika mada ya Sayari Dunia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuthibitisha kwa ufupi kauli kuwa, “Jua ni uhai” kwa kutoa hoja nne kuonesha umuhimu wa Jua kwa viumbe hai. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa, asilimia 99.2 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 4





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 97.5 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 1.7 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5 na asilimia 0.8 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama 0 hadi 1.5.


Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, asilimia 97.5 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kutoa hoja zilizothibitisha kauli kuwa “Jua ni uhai” kwa kutoa hoja zilizoonesha umuhimu wa jua katika maisha ya viumbe hai duniani. Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile, *umuhimu wa nishati ya jua katika uvukizi ambao husababisha mawingu na hatimaye mvua ambayo ni chanzo cha maji kwa mimea na wanyama*. Watahiniwa hao pia walitoa hoja kama vile, *umuhimu wa nishati ya jua katika utengenezaji wa chakula cha mimea ambayo nayo ni chakula cha viumbe hai wengine kama vile wanayama na binadamu*. Watahiniwa hao pia waliweza kuelezea umuhimu wa nishati ya Jua katika *kusaidia miili ya binadamu kupata vitamini D.*

Aidha, watahiniwa walieleza umuhimu wa Jua katika matumizi mbalimbali kama vile kukausha nafaka na nguo. Watahiniwa pia walieleza umuhimu wa j*ua katika kuleta joto ambalo linawezesha viumbe hai kuishi bila kuathiriwa na baridi kali*. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza *matumizi ya nishati ya jua katika kutengeneza nishati ya umeme kwa ajili ya matumizi mbalimbali*. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kutoa hoja zote nne kwa usahihi.


4. i) Husaidia kukausha mazao na nguo.
- Uwepo wa jua husaidia mazao kukauka na kupata chakula. Pia jua husaidia kukausha nguo.


ii) Ni chanzo cha vitamini D.
- Jua la asubuhi ni muhimu kwa afya ya binadamu kwa sababu hutupatia vitamini D kati ka miili yetu.

iii) Ni chanzo cha nishati.
- Jua ni muhimu katika maisha ya viumbe hai kama binadamu kwa sababu huzalisha nishati ya umeme Mfano wa matumizi ya Sola zinazotumia nishati ya jua.


iii) Utumika katika usanisilaji wa cha kula cha mmea.
- Ili mmea uweze kujitengenezea chakula chake Jua linahitajika.

Kielelezo Na.6. Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, katika swali hili sababu kubwa ya watahiniwa wachache (1.7%) kuwa na ufaulu wa wastani ilikuwa ni kutoa hoja chache kuliko zilizokuwa zinatakiwa na wengine kutoa hoja bila kuelezea ni kwa namna gani jua ni uhai. Vivyo hivyo, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walitoa dondoo pungufu ambazo hazikuwa na ufafanuzi wowote hivyo kuwafanya wapate alama za chini. Wengine waliotoa baadhi ya hoja ambazo hazikuwa sahihi na hivyo kutopata alama kabisa. Watahiniwa hao walitoa majibu kama vile, *Jua ni chanzo endelevu* bila kufafanua ni chanzo cha nini. Wengine waliandika majibu kama vile, *jua halitumii gharama, jua husaidia kuimarisha mifupa, hutoa mwanga, husaidia kufanya shughuli mbalimbali.* Pamoja na kwamba ni kweli Jua hutoa mwanga lakini bila maelezo ya ziada ya namna mwanga unavyowesha viumbe hai kuishi jibu linakuwa halijitoshelezi. Hii ni kwa sababu sayari zote hupata mwanga lakini mpaka sasa sayari inayojulikana kuwa na uhai ni Dunia pekee. Vile vile jibu kwamba Jua husaidia watu kufanya shughuli mbalimbali ni la jumla mno na halioneshi namna shughuli hizo zinavyowezesha uhai kuwepo. Kilelezo Na. 7 kinavyoonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.


4. i) Husaidia kuendesha shughuli mbalimbali za binadamu.
ii) Ni sayari inayowasaidia watu kuishi.
iii) Kukaushia mazao
iv) Huwasaidia kupata nishati ya joto.


Kielelezo Na.7: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa dondoo bila ufafanuzi katika swali la 4.

Katika kielelezo Na 7, mtahiniwa alieleza katika hoja ya kwanza umuhimu wa jua katika kuendesha shughuli mbalimbali bila kubainisha shughuli hizo. Aidha, katika hoja yake ya pili, mtahiniwa alichanganya Jua na sayari kwa kusema ni sayari inayosaidia watu kuishi. Kimsingi Jua siyo sayari kwa hiyo hicho kilikuwa ni kiashiria kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa mzuri kuhusu namna Jua

linavyowezesha kuwepo kwa uhai duniani. Mtahiniwa pia alitoa dondoo zingine bila kufafanua.

### 2.1.5 Swali la 5. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa; (a) kueleza dhana ya kipimo cha ramani; (b) (i) kuwakilisha 1:25,000,000 na 1:2,500,000 kwa njia ya sentensi, (ii) kubainisha aina ya kipimo ambacho kipimo cha ramani 1:25,000,000 kipo na (iii) kutaja ni kipimo kipi kati ya 1:25,000,000 na 1:2,500,000 kinaweza kutumika katika kutengeneza ramani ili iweze kuonesha vitu vingi zaidi na kutoa sababu ya majibu yake. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hilo ulikuwa hafifu. Kati ya watahiniwa waliofanya swali hilo, asilimia 37.0 ndio walikuwa na ufaulu wa alama 2 hadi 4 kama Chati Na.5 inavyoonesha.





**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5.*

Kama Chati Na. 5 inavyoonesha, asilimia 73.0 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5. Kati yao, watahiniwa asilimia 24.5 walipata alama 0. Asilimia 16.8 walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 10.2 ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri cha alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu yawezekana walikuwa na uelewa mdogo hasa kuhusu kipimo cha ramani. Watahiniwa hao walishindwa

kueleza kwa ufasaha dhana ya kipimo cha ramani katika kipengele (a). Walishindwa pia kukokotoa ili kuwasilisha kipimo 1:25,000,000 na 1:2,500,00 kwa njia ya sentensi katika kipengele (b) (i). Kwa mfano, katika kujibu swali hilo, mtahniwa mmoja alieleza kipimo cha ramani kuwa, *ni tofauti iliyopo kati ya umbali uliopo kwenye ardhi iliyopo pamoja na ukubwa au umbali wa ramani iliyochorwa.* Mtahiniwa mwingine aliandika kuwa; *kipimo cha ramani ni kipimo kinachoonyesha ukubwa wa kipimo katika ramani.* Watahiniwa hao walitarajiwa kueleza kuwa kipimo cha ramani ni uhusiano uliopo kati ya umbali katika ramani na umbali halisi katika ardhi.

Katika kipengele (b) (i) watahiniwa walishindwa kubadili vipimo vya ramani vilivyowasilishwa kwa njia ya uwiano kuwa katika njia ya sentensi. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walikosea kukokotoa hivyo kusababisha kupata majibu yasiyo sahihi. Katika kipengele (b) (ii) watahiniwa walishindwa kubainisha aina ya kipimo ambacho 1:25,000,000 kinawakilisha. Watahiniwa wengi katika kundi hili walibainisha kipimo 1:2,500,000 kama kipimo kikubwa kutokana na 25,000,000 kuwa namba kubwa. Watahiniwa pia walishindwa kubainisha ni kipimo kipi kati ya 1:25,000,000 na 1:2,500,000 kinaweza kutumika kuwasilisha vitu vingi zaidi kwenye ramani. Wengi wa watahiniwa walichagua 1:25,000,000 bila kufahamu kuwa, kipimo hicho kinawasilisha eneo kubwa la ardhi kwenye ramani na hivyo ramani inayotokana na kipimo hicho inaonesha vitu vya jumla tu. Kielelezo Na. 8 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.


5. a) Kipimo cha ramani ni dhana inayo tumika kupima urefu na upana katika ramani

b i) Kilometa moja ni sawa na sentimita 25 1000000 katika uso wa dunia

ii) Kinaonesha uwiano

iii) Kipimo kinachoweza kutengeneza ramani ili iweze kuonesha vitu vingi zaidi ni 1:2500000 kwa sababu kipimo kidogo cha ramani huonesha eneo kubwa katika ramani

Kielelezo Na. 8: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5


Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kukosea vipengele vingine. Katika kundi hili, baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza dhana ya kipimo cha ramani kwa usahihi lakini walishindwa kubadili vipimo vilivyowasilishwa kwa njia ya uwiano kuwa katika njia ya sentensi. Watahiniwa wengine walishindwa kubainisha aina ya kipimo katika kipengele (b) (ii), licha ya kuweza kueleza dhana ya ramani na kuweza kubadili vipimo na kuviwasilisha kwa njia ya sentensi katika kipengele (b) (i). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi kipengele (a) kwa kuandika kuwa, *kipimo cha ramani … ni uhusiano kati ya umbali halisi katika uso wa dunia na umbali katika ramani.* Mtahiniwa huyo pia alibadili vipimo vilivyowasilishwa kwa njia ya uwiano na kuwa katika njia ya sentensi lakini alishindwa kipengele cha (iii) chote.

Kwa upande mwingine, asilimia 10.2 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na uelewa mzuri wa mada ya stadi sahili na tata za picha na ramani hasa eneo la kipimo cha ramani. Wengi wa watahiniwa katika kundi hili waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi isipokuwa wengi wao walishindwa kutoa sababu katika kipengele (iii). Kielelezo Na. 9 ni sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mojawapo ya watahiniwa waliofanya vizuri katika swali hilo.

05 (a) Kipimo cha ramani ni uwiano uliopo kati ya umbali kwenye ramani na umbali wa kitu halisi katika uso wa dunia

b)(i) 1: 25 000,000
Sm 1 = km 100000
sm 25000000.
Sm 1 kwa kilometa 250

(ii) sm 1 = km 100000
sm 2500000
= sm 1 kwa kilometa 25



05 (ii) Kipimo kidogo cha ramani


(iii) 1:2,500,000

Kielelezo Na. 9: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5

Kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 9, mtahiniwa aliweza kijibu vizuri vipengele vyote. Hata hivyo, katika kipengele cha (iii) mtahiniwa aliandika kipimo 1:2,500.000 kinaweza kuonesha vitu vingi zaidi ya kingine bila kutoa sababu.

### 2.1.6 Swali la 6. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika

Swali la 6 lilitungwa kutoka katika mada ya Vitangilizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi kwa kutoa hoja nne ni kwa nini Wapelelezi, Wamisionari na Wafanyabiashara waliitwa vitangulizi vya ukoloni. Katika kujibu swali hili, mtahiniwa alitakiwa kufahamu namna ambavyo kila kundi lilisaidia katika kuwezesha mataifa ya Ulaya kulitawala Bara la Afrika. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa wastani kwani asilimia 64.9 ya watahiniwa ndio walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri (alama 2 hadi 4) kama inavoonekana kwenye Chati Na. 6.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa kati ya watahiniwa waliofanya swali hilo, asilimia 25.9 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 39.0 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5 na asilimia 35.1 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutoa sababu zilizojitosheleza kuelezea sababu za wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara waliitwa vitangulizi vya ukoloni. Katika maelezo yao watahiniwa walitoa hoja kama vile, kukusanya taarifa mbalimbali za jamii za Afrika kama hususan utamaduni, ulinzi na usalama wa jamii, maliasili zilizokuwepo kwenye jamii hizo pamoja na hali ya hewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa, *wapelelezi waliwapeleleza waafrika na viongozi wao, tamaduni zao na maisha yao kabla ya kuanzishwa kwa ukoloni.* Kwa kuwa haya yote yalifanyika kabla ya ukoloni, taarifa hizo zilitumiwa na mataifa ya Ulaya kubuni namna ya kulitawala bara la Afrika.

Katika kujenga hoja kwa nini wamisionari waliitwa vitangulizi vya ukoloni mtahiniwa mwingine alieleza kuwa, *waliitwa vitangulizi vya ukoloni kwa sababu walikuja kueneza dini ya kikristo ili kulainisha mioyo ya waafrika.* Wafanyabiashara wanahusishwa na ukoloni kwa kuwa waliunda makampuni ambayo baadaye yalitumiwa na serikali ambako wamiliki walitoka kuzitawala nchi za kiafrika. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa watahiniwa wengi katika kundi hili walishindwa kutoa hoja madhubuti zinazodhihirisha sababu za makudi hayo kuitwa vitangulizi vya ukoloni. Kielelezo Na. 10 ni sampuli ya majibu sahihi ya swali la 6.




6. Wapelelezi, wamisionari na wafanya biashara waliitwa vitangurizi vya ukoloni kwa sababu.
(i) walitumwa kuja kupeleleza maisha ya waafrika kwa ujumla na raslimali walizonazo 1
(ii) Walikuja kueneza dini ya kikristo ili kurainisha mioyo ya waafrika (wamisionari)
(iii) Walikuja kutafuta marighafi na kuwekeza mitaji yao kutokana na huko kwao kulikuwa na ongezeko la watu
(iv) Walikuja kwa lengo la kukomesha biashara ya utumwa na kuanzisha biashara zao pamoja na mashamba ya kilimo (wafanyabiashara)

Kielelzo Na. 10: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 6

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili walikuwa na dosari katika majibu yao. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitoa hoja pungufu na wengine walishindwa kutoa sababu ziliazojitosheleza. Walieleza sababu za kulivamia na kuligawa bara la Afrika, badala ya kueleza mambo yaliyofanywa na wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara kama maandalizi ya uvamizi na hatimaye kutawaliwa kwa bara la Afrika.

Kwa upande mwingine, majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu yanaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo waliyofanya wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara ambayo yaliandaa mazingira kwa mataifa ya Ulaya kulivamia Bara la Afrika. Hivyo, hoja zao hazikujikita katika kujenga sababu za watu hao kuitwa vitangulizi vya ukoloni badala yake waliandika hoja ambazo hazikuzingatia mahitaji ya swali kama kielelezo Na. 11 kinavyoonesha.


6. i/. Walikuwa watu wa kwanza kufika Afrika.
- Hii ina maana kwamba wapelelezi, wamisionari pamoja na wafanyabiashara hawa ndo walikuwa watu wa kwanza kufika Afrika.

ii/. Walianzisha biashara ya watumwa.
Wapelelezi, wamisionari pamoja na wafanyabiashara waliitwa vitangulizi vya ukoloni kwasababu walianzisha biashara za utumwa.

iii/. Walianzisha mambo ya unyonyaji.
Hii ina maana kwamba wapelelezi, wamisionari pamoja na wafanyabiasha waliitwa vitangulizi vya ukoloni kwasababu walianzisha mambo ya unyonyaji.

iv/. Walianzisha mambo ambayo wakoloni walikuja kuyaendeleza.
- Wapelelezi, Wamisionari na wafanyabiashara waliitwa vitangulizi vya ukoloni kwasababu walianzisha mambo ambayo wakoloni


Kielelzo Na. 11: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6

Kielelezo Na.11 kinaonesha kuwa, mtahiniwa katika hoja yake ya kwanza aliandika waliitwa vitangulizi kwa sababu walikuwa wa

kwanza kufika Afrika. Ingawa huo ni ukweli, lakini hawaitwi hivyo kwa kuwa tu walikuwa wa kwanza kufika Afrika bali mambo waliyojishughulisha nayo ambayo yaliandaa mazingira ya ukoloni. Katika hoja ya pili mtahiniwa aliandika walianzisha biashara ya utumwa kitu ambacho siyo kweli. Kimsingi baadhi yao walipinga biashara ya utumwa.

### 2.1.7 Swali la 7: Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira. Katika kujibu swali hili, mtahiniwa alitakiwa apambanue mabadiliko yaliyojitokeza wakati wa Zama za Chuma ikilinganishwa na wakati wa Zama za Mawe kwa kutoa hoja nne. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 97.3 walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ambapo asilimia 63.9 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 33.4 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 2.7 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha. Waliweza kuchanganua kwa usahihi mabadiliko yaliyojitokeza

wakati wa Zama za Chuma ikilinganishwa na Zama za Mawe. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja kama vile, *uzalishaji mali uliongezeka kutokana na kubuniwa kwa zana bora zaidi za uzalishaji mali ikilinganishwa na zana za mawe zailizotumika wakati wa Zama za Mawe*. Watahiniwa hao pia walitoa hoja kama vile w*atu kuanza kuishi kwenye Makazi ya kudumu* tofauti na wakati wa Zama za Mawe ambapo *watu waliishi kwa kuhamahama kulingana na upatikanaji wa chakula kama vile matunda mwitu*. Watahiniwa pia waliweza kueleza *kuibuka kwa tabaka la wakulima na wahunzi*. Kuibuka kwa matabaka hayo kulisababisha kuanza kwa biashara kati yao. Mfano wa majibu sahihi yaliyoandikwa na watahiniwa ni kama yafuatayo:

*(i) Kwenye Zama za Chuma kulikuwa na mgawanyo wa kazi, ukilinganisha na kwenye Zama za Mawe kulikuwa hakuna mgawanyo wa kazi.*

*(ii) Zama za Chuma uzalishaji uliongezeka na hiyvo watu kupata chakula cha kutosha ukilinganisha na Zama za Mawe kulikuwa hakuna uzalishaji bali watu walitumia matunda na mizizi kama chakula chao.*

*(iii) Kwenye Zama za Chuma kulikuwa na zana bora za kilimo na hivyo kuwarahisishia katika uzalishaji wao ukilinganisha na kwenye Zama za Mawe kulikuwa hakuna zana bora bali walitumia mawe kama zana zao za kuwasaodia katika uchimbaji wa mizizi.*

*(iv) Katika Zama za Chuma watu waliishi kwenye makazi ya kudumu, walijenga nyumba ukilinganisha na kwenye Zama za Mawe ambapo binadamu aliishi kwa kuhamahama.*

Mtahiniwa mwingine alijibu swali hilo kwa kuandika kuwa;


*(i) Wakati wa zama za Mawe, watu waliishi kwa kuhamahama wakati katika Zama za Chuma watu walianza kuishi katika makazi ya kudumu*

*(ii) Waakati wa Zama za Mawe watu walikuwa vyakula vibichi wakatii katika Zama za Chuma watu walikula kilichopikwa au kuchomwa.*

*(iii)* *Katika zama za Mawe, watu walitumia zana duni mfano mawe wakati katika Zama za Chuma watu walitumia zana bora mfano mikukina visu*

*(iv)* *Wakati wa Zama za Mawe watu walikuwa na uwezo mdogo wa kufikiri lakani wakati wa Zama za Chuma watu walikuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri.*

Majibu haya ya watahiniwa katika kundi hili yalionesha wazi kuwa walielewa walichotakiwa kufanya wakati wa kujibu swali hilo. Aidha, majibu ya aina hii ni kielelezo kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri kuhusu zama mbalimbali katika maendeleo ya binadamu na matukio yaliyotokea katika zama hizo. Kielelezo Na. 12 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo aliyejibu vizuri swali hilo na kupata alama zilizomwezesha kufaulu vizuri.


7 i) Wakati wa zama za mawe wali kuwa wanatumia zana duni lakini wakati wa zama za Chuma wali tumia zana bora.

ii) Wakati wa zama za mawe walikuwa wanaishi [illegible] kwa [illegible] lakini katika zama za chuma [illegible]

iii) Wakati wa zama za mawe walikuwa na zana [illegible] lakini katika zama za chuma walikuwa na zana [illegible]

iv) Wakati wa zama za mawe walikuwa wanatafuta chakula kwa kuwinda, [illegible] lakini wakati wa zama za Chuma walianza [illegible] ya chakula

Kielelezo Na.12: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7


Kwa upande wa watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani, majibu yao yalionesha upungufu wa maarifa katika kuhusisha matukio na

zama yalizotokea. Baadhi yao waliandika hoja pungufu hivyo kutopata alama za kuweza kufaulu vizuri. Uchambuzi unaonesha pia watahiniwa hao walirudia baadhi ya hoja kwa maneno tofauti kama hoja tofauti kitu kilichofanya wakose baadhi ya alama.

Katika swali hili, kulikuwa na watahiniwa wachache (2.7%) ambao walikuwa na ufaulu hafifu. Sababu kubwa ya watahiniwa hao kuwa na ufaulu hafifu ni kutoa hoja pungufu na wengine kuandika majibu bila kupambanua matukio kati ya zama hizo. Kwa mfano, katika kujibu swali hilo, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yake kama ifuatavyo;

*(i)* *Binadamu alianza kuwinda*
*(ii)* *Aligundua moto*
*(iii)* *Binadamu alianza (***mtahiniwa hakumalizia sentensi***)*

Majibu haya ya mtahiniwa yanaashiria vitu viwili. Kwanza, mtahiniwa hakuwa na maarifa mahsusi kuhusi Zama za Chuma ikilinganishwa na Zama za Mawe. Pili yawezekana muda wa mtihani ulikuwa umekaribia kwisha hivyo akaamua kuandika dondoo tu badala ya kuandika majibu kikamilifu. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliandika majibu ambayo yaliashiria kuwa hawakuwa wameelewa walichotakiwa kufanya hivyo kutoa majibu ambayo hayakuendana na swali kama Kielelezo Na. 13 kinavyoonesha.



7 i/ Kuwepo kwa uongozi mubaya uliopo madara kani
ii/ Kutokuwepo kwa maendeleo ya kutosha kutoka na na uwepo wa chama kimoja
iii/ ili kuleta changamoto ya kisiasa ~~kati~~ ambayo huppelekea uwepo wa maendeleo.
iv/

Kielelezo Na. 13: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7

Majibu ya mtahiniwa katika kilelelezo Na. 13 hayana uhusiano wowote na swali. Swali linataka kupambanua mabadiliko yaliyojitokeza wakati wa Zama za Chuma ikilinganishwa na mabadiliko yaliyotokea wakati wa Zama za Mawe. Kwenye majibu ya mtahiniwa hakuna jibu lolote linaloongelea nyakati hizi mbili.

### 2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii baada ya Afrika Huru

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii baada ya Afrika huru. Katika kujibu swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja nne akieleza ni kwa nini nchi nyingi za kiafrika zilifuata mfumo wa vyama vingi mwanzoni mwa miaka ya 1990. Ufaulu katika swali hilo kwa ujumla ulikuwa hafifu kutokana na asilimia 13.6 tu ya watahiniwa kupata alama 2 hadi 4 kama Chati Na. 8 inavyoonesha.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika swali la 8.*

Takwimu katika Chati Na. 8 zinaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliofanya swali hilo, asilimia 86.5 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa wengine asilimia 8.9 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5 na asilimia 4.7 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, majibu ya asilimia 86.5 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuzingatia matakwa ya swali. Wengi wao walieleza mambo yanayoonekana kuwa ni manufaa ya nchi za kiafrika kufuata mfumo wa vyama vingi badala ya kueleza mambo yaliyosababisha nchi hizo kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi kipindi cha miaka ya 1990. Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile, kuepuka baadhi ya viongozi

kung'ang'ania madaraka kwa muda mrefu, kuwapa uhuru wananchi wa kushiriki katika uamuzi katika mchakato wa kupata viongozi, na kuchochea ushindani ambao unaleta maendeleo. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alijibu kwa hoja zifuatazo;

(i) *Kuleta ushindani katika maendeleo. Hii inatokea sababu chama kikiwa kimoja viongozi wake watakaa bila kuleta maendeleo kwa wananchi wake laknii vyama vikiwa vingi lazima vitahoji kuhusu maendeleo*

(ii) *Kutetea haki za binadamu. Katika nchi ambayo kuna vyama vingi, inalinda na kutetea haki a binadamu kwa sababu hao watu ndiyo waliowachagua.*


(iii) *Kulinda mali za umma. Mfumo wa vyama vingi husaidia kulinda mali za umma zisipotee au kusije tokea mtu mmoja akzitumia kwa maslahi yake biinafsi.*

(iv) *Kupambana na rushwa. Katika nchi zenye mfumo wa vyama vingi hupambanan na rushwa ambayo inawea kuleta migogoro katika jamii na taifa zama kwa ujumla.*

Mtahiniwa mwingine katika kujibu swali hilo alito hoja zifuatazo;

(i) *Kuleta maendeleo (ii) kupunguza rushwa (iii) kulinda haki za binadamu na (iv) kushauri serikali iliyopo madarakani.*

Majibu ya mlengo huu yameonekana kwa watahiniwa wengi wenye ufaulu hafifu. Pamoja na kwamba mambo haya ni muhimu, hayakuwa chanzo cha nchi nyingi kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa hao ama hawakusoma kwa makini na kuelewa swali linataka nini au hawakuwa na maarifa kuhusu mambo ambayo yalisababisha nchi nyingi za kiafrika kuingia katika mfumo wa vyama vingi katika miaka ya 1990. Kilelelzo Na. 14 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi.


08. Umuhimu wa Mfumo Vyama Vingi:
(i) Ili kutoa uhuru wa kila mtu kumchagua kiongozi anayempenda.
(ii) Ili kutoa uhuru wa mtu yeyote kugombea nafasi za uongozi ndani ya nchi.
(iii) Ili kuleta ushindani wa kimaendeleo.
(iv) Ili kukuza mfumo wa siasa katika nchi zao.


Kielelezo Na. 14: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8

Mtahiniwa katika majibu yake ameeleza umuhimu wa mfumo wa vyama vingi badala ya kueleza sababu za nchi nyingi za kiafrika kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi. Kwa ujumla, hoja alizozieleza zinaangukia kwenye jambo moja la madai yaliyokuwa yakitolewa na wasomi mbalimbali wa kiafrika ambao nao walikuwa wakishinikiza kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani umeonesha kuwa, walichanganya baadhi ya hoja zilizohusu umuhimu wa kuanzishwa kwa vyama vingi, na hoja zilizohusu sababu zilizofanya kuanzishwa kwa mfumo huo katika mataifa ya kiafrika. Mchanganyiko huo wa hoja ulisababisha watahiniwa hao kupata alama za wastani (kati ya 2 haid 2.5) kati ya alama 4 za swali hilo.

Asilimia 4.7 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutoa hoja tatu sahihi, na hoja moja ambayo haikuwa sahihi sana lakini ilizungumzia sababu ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi barani Afrika katika miaka ya 1990. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja kama vile, *Msumkumo kutoka shirika la Fedha Duniani (IMF), msukumo wa Benki ya Dunia wa kuzitaka nchi za Kiafrika kupanua wigo wa kidemokrasia katika nchi zao*; *Msukumo kutoka nchi tajiri duniani kama vile Marekani na nchi za Ulaya uliozishinikiza nchi za Kiafrika kufuata mfumo wa vyama vingi vinginevyo zingeacha kuzifadhili*; *Kusambaratika kwa dola ya siasa ya Ujamaa iliyokuwa chini ya Urusi ambaye alikuwa ndiyo mama wa chama kimoja.* Hoja zingine kama vile uwepo wa vuguvugu la wasomi katika nchi za Kiafrika ambao waliongoza madai ya mabadiliko kwa kufanya mikutano na makongamano wakionesha

umuhimu wa vyama vingi. Kilelezo Na. 15 kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa.



8 ii) Tishio la kutopewa msaada wowote kutoka kwa mataifa yanayotumia mfumo huu.
iii) Madai kutoka benki ya dunia kwamba taifa ambalo halikufuata mfumo lilipata vikwazo katika kukopa fedha.
iv) Maendeleo duni, na malalamiko ya raia pamoja na vyama vya siasa kudai uhuru wa demokrasia

Kielelezo Na. 15: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la *8*.

Mtahiniwa katika hoja zake aliweza kueleza mbadiliko yaliyotokea ambayo yalizilazimu nchi za kiafrika kuingia katika mfumo wa vyama vingi katika miaka ya 1990. Hata hivyo, hoja yake ya mwisho ina dosari ndogo alipoandika kuwa kulikuuwa na malalamiko kutoka vyama vya siasa ambavyo kwa wakati huo havikuwepo. Lakni ni kweli kuwa kulikuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya raia hasa wasomi waliokuwa wakiishi ndani na hasa nje ya nchi hizo ambao walishinikiza kuanzishwa kwa vyama vingi.

### 2.1.9 Swali la 9: Mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii baada ya Afrika Huru


Swali hili lilitungwa kutoka mada ya Mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii baada ya Afrika huru. Katika kujibu swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi mafanikio manne ya kijamii yaliyofikiwa na serikali za kiafrika baada ya kupata uhuru. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, kwa ujumla, ufaulu katika swali hilo ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 84.4 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 9 inaonesha kwa muhtasari ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Kama Chati Na. 9 inavyoonesha, asilimia 59.3 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilmia 25.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadii 2.5 na asilimia 15.6 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5 ambapo asilimia 2.9 kati yao walipata 0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza kwa kifupi mafanikio ya kijamii yaliyofikiwa na nchi za kiafrika baada ya uhuru. Watahiniwa hao waliweza kubainisha maeneo ambayo mataifa ya kiafrika yamepiga hatua kama vile *ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, maendeleo katika sekta ya elimu kama vile ujenzi wa shule, vyuo vya kati na vyuo vikuu, mafanikio katika sekta ya afya ikiwemo ujenzi wa zahanati na hospitali za ngazi mbalimbali*. Kielelezo Na. 16 ni mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa mmojawapo katika kundi hili.


09. I. Elimu, elimu kwa kasi kikubwa iliweza kutolewa kwa watu wengi bila kuwepo kwa ubaguzi wa rangi.

II. Huduma ya Afya, hapa zahanati, mahospitali yaliweza kujengwa kwa ajili ya kutoa huduma ya afya


III. Mawasiliano, baada ya uhuru mawasiliano yaliweza kukuwa kwa kasi kubwa.

IV. Maji, mabomba mbalimbali yaliweza kutumika kusafirishia maji kupatikana katika sehemu tofautitofauti.

Kielelezo Na. 16: Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 9.

Uchambuzi wa majibu ya asilimia 25.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani umeonesha kuwa, watahiniwa hao walichanganya hoja zilizoelezea mafanikio yaliyofikiwa na nchi za kiafrika baada ya uhuru. Baadhi yao pia waliandika hoja ambazo zilielezea mafanikio ambayo hayakuwa bayana hivyo, kupata alama pungufu. Wengine walieleza hoja zilizohusu mafanikio ya kisiasa na ya kiuchumi badala mafanikio ya kijamii kama swali lilivyouliza.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walitoa hoja zisizoridhisha. Watahiniwa hao walitoa hoja ambazo hazikuonesha tofauti kubwa iliyokuwepo wakati wa ukoloni na mabadiliko yaliyotokea baada ya uhuru. Watahiniwa wengine walichanganya hoja zinazohusu mafanikio ya kisiasa na mafanikio ya kiuchumi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *(i) Kupata nafasi ya kujiongoza wao wenyewe kwa uhuru (ii) kukuza na kuboresha utamaduni pamoja na kijamii (iii) kupata nafasi ya kujitegemea kiuchumi pamoja na kijamii (iv) Nchi kufaidika na rasilimali zake.* Mtahiniwa mwingine aliandika kama ifuatavyo: *(i) Kupatikana kwa huduma za kijamii kwa urahisi.* Katika jibu hili mtahiniwa hakueleza ni huduma zipi. *(ii) serikali kuwa huru katika kuamua mambo yake bila kuingiliwa (iii) kupatikana kwa hali ya Amani na utulivu katika nchi*. Majibu (ii) na (iii) ya mtahiniwa ni mafanikio ya kisiasa kinyume na swali lililohitaji mafanikio ya kijamii. Keielelezoo Na. 17 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi la mtahiniwa mmojawapo katika kundi hilo.


9 (i) Jamii kuwa na uhuru wa kulima mazao
ya chakula na biashara
kabla ya uhuru jamii ya Afrika walikuwa
hawana uhuru wa kulima mazao ya chakula.

(ii) Usawa kwa kila jamii
Baada ya uhuru wa mwa 1961 jamii ya Afrika
ili anzisha usawa kwa kila mwafrika bila ya
kunyanyaswa.

(iii) kuboreshwa kwa huduma za kijamii Mfano
Hospitali na shule
Baada ya uhuru elimu na huduma ya afya
haikuwa ya ubaguzi kama mwanzo kabla
ya uhuru.
(iv) Uchumi uli anza kuongezeka (kukua)
uchumi uliongeza kwa sababu jamii ilikuwa ku


Kielelezo Na. 17: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 9.

Katika kielelezo Na. 17 majibu ya mtahiniwa yalikuwa na dosari katika hoja zake na hivyo kupata alama hafifu. Kwa mfano, katika hoja ya kwanza mtahiniwa anaeleza kuwa moja ya mafanikio ya nchi za kiafrika ni uhuru wa kulima mazao ya chakula na ya biashara. Hoja hiyo haikuwa na nguvu kwa sababu, watu katika mataifa mengi ya Afrika waliendelea kulima mazao ya biashara yaliyoletwa na wakoloni kama vile pamba, kahawa na chai. Aidha, wananchi waliendelea kulima mazao yao ya asili. Kwa hiyo hapakuwa na ukosefu wa uhuru ambao mtahiniwa alikuwa anajaribu kuuelezea. Ingawa mtahiniwa alikuwa sahihi katika hoja ya tatu (iii) *kuboreshwa kwa huduma za kijamii kama hospitali na shule,* suala la usawa katika hoja ya pili haliwezi kuwa moja ya mafanikio yaliyopatikana wakati ambapo bado jamii nyingi katika bara la Afrika zinaendelea na jitihada za kuhimiza usawa katika jamii. Majibu ya aina hii ndiyo hasa yaliyofanya watahiniwa wengi kwenye kundi hili kuwa na ufaulu hafifu.

### 2.1.10 Swali la 10: Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni.* Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa kifupi sababu nne za kuzuka kwa vita vya Majimaji kama hatua ya watu wa Tanganyika kupinga utawala wa kikoloni.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo kwani asilimia 92.6 walipata alama kati ya 2 hadi 4 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 10.





**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Takwimu katika Chati Na. 10 zinaonesha kuwa, asilimia 77.9 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 14.7 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5 na asilimia 7.4 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa asilimia 77.9 ya watahiniwa ulitokana na watahiniwa hao kuweza kutoa sababu tatu hadi nne kwa usahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni na hasa chimbuko la vita vya Majimaji. Watahiniwa hao walieleza kero mbalimbali walizozipata wananchi ambazo zilisababisha washike silaha ili kupinga utawala wa kikoloni.

Hoja zilizojitokeza zaidi kwa watahiniwa walio wengi ni pamoja na *kupinga kunyang'anywa ardhi yao ambayo walikuwa wakiitumia kwa kilimo*; *kupinga ubaguzi wa rangi kwa kuwa waafrika walikuwa hawathaminiwi*, *kupinga kulipa kodi kwa serikali ya kikoloni; kupinga kufanyishwa kazi kwenye mashamba ya wakoloni bila ujira au kwa ujira mdogo sana* pamoja na *kupinga unyanyasaji waliokuwa wakifanyiwa kama vile kuchapwa viboko hadharani.* Kielelezo Na.

18 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa mmojawapo katika hilo kundi.


10 i) waafrika walichoka kulazimisha kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni. Mfano mashamba ya kahawa, miwa na pamba.
ii) kupokonywa kwa ardhi zenye rutuba; pia ilipelekea kuzuka kwa vita vya majimaji kwa sababu waafrika walichoka kutawaliwa kinabavu.
iii) Ulipishwaji wa kodi uliokithiri. Mfano wa kodi ni kodi ya kichwa na kodi ya matiti. hii kodi ilikua inatolewa pale tu mtoto wa kike ameshaanza kuota matiti.
iv) Upolwaji wa Malighafi: Mfano kahawa, pamba na katani.


Kielelezo Na.18: Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 10.

Majibu ya mtahiniwa katika Kielelezo Na. 18 liligusia maeneo yote ambayo waafrika yaliwakera kiasi cha kuamua kupinga ukoloni kwa njia ya vita. Hata hivyo, hoja yake ya nne siyo sahihi sana kwa kuwa walichokuwa wanapinga wananchi wakati huo ni kulima mazao yaliyoletwa na Wajerumani kama mazao ya biashara. Wao hawakuona umuhimu wake kwa hiyo wakawa wanapinga kulima mazao hayo.

Asilimia 14.7 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliweza kueleza hoja mbili kwa ufasaha na kueleza hoja nyingine mbili ambazo hazikuwa zinajibu swali kikamililifu. Baadhi ya watahiniwa walieleza masuala ya kupinga utumwa. Watahiniwa hao walichanganya dhana ya kupinga utumwa na dhana ya kupinga ukoloni. Biashara ya utumwa ilikuwa imeshasitishwa kabla ya ukoloni hivyo hoja kama hizo hazikuwa zinaendana na matakwa ya swali. Aidha, baadhi ya watahiniwa walitoa maelezo ya jumla kama vile kupinga unyonyaji bila kubainisha aina ya unyonyaji ambao waafrika walipinga hivyo kusababisha kupata alama hafifu.

Watahiniwa wachache (7.4%) waliokuwa na ufaulu hafifu kwenye swali hilo walitoa majibu ambayo yalionesha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu chimbuko la vita vya Majimaji na hivyo kuwafanya washindwe kutoa hoja zilizoendana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa dondoo zifuatazo; *(i) mila potofu za waafrika (ii) kupinga uvamizi (iii) sababu za kisiasa na (iv) unyonyaji uliokithiri*. Ingawa katika dondoo alizotoa ya (iv) ina ukweli ndani yake, mtahiniwa huyo hakufafanua ni

unyonyaji gani ambao Waafrika walikuwa wanaupinga dhidi ya utawala wa kijerumani. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliandika namba ya swali bila kutoa majibu yoyote, na wengine waliandika sababu zilizowafanya Waafrika kushindwa katika vita hivyo kama kielelezo Na. 19 kinavyoonesha.



| | | |
|---|---|---|
| 10 | (i) Watanganyika kuwa silaha duni ya kupiga vita | |
| | na wakoloni. | |
| | (ii) Kutokuwa na mbinu ya kupigania vita ili kupi- | |
| | nga utawala. | |
| | (iii) Uhaba wa wataalamu wa vita. | |
| | (iv) Kutokuwa na jeshi imara. | |


Kielelezo Na.19: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

## 2.2 Tathmini B: Maswali ya Insha

Sehemu B na C katika mtihani wa Maarifa ya Jamii zilikuwa na maswali sita ya insha. Sehemu B ilikuwa na maswali manne ya taaluma, mawili yalihusu somo la Jiografia na mawili somo la Historia. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua maswali mawili katika sehemu B (swali moja kwa kila somo). Sehemu C ilikuwa na maswali mawili yaliyohusu ufundishaji ambayo mtahiniwa alitakiwa kujibu yote. Kila swali katika sehemu hizi lilikuwa na uzito wa alama 15. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika mkundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa 0-5.5, 6-10.0 na 10.5-15 mtawalia.

### 2.2.1 Swali la.11: Nchi Yetu Tanzania

Swali hili lilitoka katika mada ya Nchi Yetu Tanzania. Mtahiniwa alitakiwa kufafanua mambo matano muhimu yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa uanzishwaji wa kiwanda. Swali lilijibiwa na watahiniwa 2,098 sawa na asilimia 71.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Swali hilo lilikuwa moja ya maswali yenye ufaulu mzuri kwa kuwa asiliimia 99.3 ya watahiniwa walipata alama 6.0 hadi 15. Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliofanya swali hili, asilimia 83.0 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14.5, asilimia 16.3 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10.0 na asilimia 0.7 tu ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kufafanua kwa ufasaha mambo muhimu yanayohitajika wakati wa kuanzisha kiwanda. Mambo ambayo watahiniwa wengi waliyagusia ni pamoja na; *upatikanaji wa malighafi, uwepo wa masoko ya bidhaa zitakazozalishwa, uwepo wa wafanyakazi wenye ujuzi unaoendana na tekinolojia ya kiwanda husika, uwepo wa miundombinu mizuri ya mawasiliano na uchukuzi na sera nzuri za serikali zinazowezesha uratibu wa haraka wa taratibu za kuanzisha kiwanda*. Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri wa mahitaji ya uanzishwaji wa viwanda na hivyo, waliweza kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya swali. Kielelezo Na. 20 ni sampuli ya majibu sahihi ya mmojawapo wa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo.

11. Kiwanda ni Sehemu ambayo bidhaa huzalishwa au hutengenezwa katika kuanzisha Shughuli za Viwanda Inapaswa kuzingatia mambo mbalimbali: Pia kuna Viwanda vya uchimbaji na vingine vingi. Katika kuanzisha Viwanda Inapaswa kuzingatia.

Yafuatayo ni mambo ambayo yanapaswa kuzingatia wakati wa kuanzisha kiwanda.

Kuzingatia uwepo wa malighafi, katika kuanzisha kiwanda Inapaswa kuzingatia kuwepo kwa malighafi ya bidhaa ambayo itatengenezwa mfano katika uanzishaji kutengeneza ~~kiwanda~~ mafuta ya nazi ni lazima kuzingatia Sehemu utakayoanzisha kiwanda kuna nazi za kutosha.

Kuanzisha kiwanda kuzingatia uwepo wa maji wa kutosha: Katika kuanzisha Viwanda ni lazima kuzingatia uwepo wa maji katika Sehemu ambayo unaanzisha au maji ulionao unaweza kuanzisha kiwanda. Kwahiyo katika kuanzisha kiwanda Inapaswa kuzingatia maji.

Kuanzisha kiwanda lazima kuzingatia uwepo wa soko au wateja watakao nunua bidhaa ambayo Inazalishwa kiwandani katika kuanzisha kiwanda Inapaswa kuzingatia uwepo wa soko katika la bidhaa ambayo itazalishwa kiwandani. Pia unapoanzisha kiwanda lazima kuzingatia uwepo wa soko.

Kuanzisha kiwanda lazima kuzingatia wafanyakazi ambao watafanya kazi katika


11. kiwanda. Mfano katika kiwanda kuanzisha
lazima kuzingatia kuwepo kwa wafanyakazi
ambao watafanya kazi katika kiwanda.
Ni vizuri katika kuanzisha kiwanda
kuzingatia wafanyakazi watakaofanya kazi.
Tano, kuzingatia kama kiwanda
kina Ithibati (Leseni) ya kiwanda. Katika
kuanzisha kiwanda lazima kiwe na Leseni
ya kiwanda ambacho kitapelekea
kiwanda kufanya kazi kiutaratibu na
kisheria, hivyo kiwanda ni vema
kiwe na leseni ya biashara.
Kwahiyo katika kuanzisha
kiwanda hupaswa kuzingatia mambo
mbalimbali kama uwepo wa malighafi,
wafanyakazi, Miundombinu bora ya umeme,
ambayo, itasaidia katika uzalishaji
wa bidhaa. hivyo unapoanzisha kiwanda
ni vema kuzingatia mambo hayo.


Kielelezo Na.20: Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 11.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, asilimia 16.3 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na dosari chache kwenye majibu yao. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliandika hoja chache kuliko hoja zilizokuwa zinahitajika. Watahiniwa wengine waliandika hoja ambazo hazikuwa na mantiki, au hazikukidhi mahitaji ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuwa uanzishaji wa viwanda unahitaji; *uwepo wa bidhaa ambazo zitatumika viandani ni muhimu sana viwepo wakati wa uanzishwaji wa soko inapotaka kuanzisha kiwanda lazima kuwepo na bidhaa zinazohitajika.* Ilikuwa vigumu kuelewa mtahiniwa alikuwa anazungumzia bidhaa zipi wakati hoja ilikuwa inatakiwa kulenga uanzishwaji wa kiwanda. Mtahiniwa tayari alikuwa ameshazungumzia upatikanaji wa malighafi, hivyo hata kama neno bidhaa alimaanisha malighafi, basi ni hoja ambayo tayari alikuwa ameshaitoa. Baadhi ya watahiniwa pia walirudia hoja hivyo kuwafanya kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili walieleza mambo ambayo nayo yanahitajika kiutaratibu wakati wa kuanzisha viwanda, lakini ni mambo ambayo yakikosekana hayawezi kuathiri uanzishwaji wa kiwanda. Ingawa ni kweli kuwa uendeshaji

wa kiwanda unahitaji kuzingatia mambo mbalimbali kama vile utunzaji wa mazingira, uhitaji wa leseni ya kuendeshea shughuli za viwanda; lakini hayana uzito mkubwa katika uwepo wa kiwanda hicho ikiwa kiwanda kinachoanzishwa hakitakuwa na malighafi, uwepo wa nishati, mtaji, na masoko. Majibu kama hayo yalifanya watahiniwa kupata alama hafifu kutokana na kuacha kugusia mambo ambayo ni muhimu zaidi. Kielelezo Na. 21 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na ufaulu hafifu.


11. Kiwanda; Ni mahali auvche
mu ambapo upelekwa malighafi
ili ziweze kuchakatwa na kute
ngeneza bidhaa tayari kwa mauzo.
Yanayotayo ni mambo ya
kuzingatia wakati wa kuanzishwa
kiwanda nayo ni:
Eneo la ujenzi; Linatakiwa
liwe mbali na makazi ya watu ili
kuepusha athari zitokanazo na
uzalishaji wa kiwanda.
Afya za wananchi; Kiwa
nda kinatakiwa kizingatie afya za
wananchi wanaoishi katika
maeneo yale ili kuepukana na
madhara mbalimbali.


Usafi wa Mazingira; Mfano uwepo wa mitaro inayopeleka maji sehemu inayotakiwa ili kuzuia mlipuko wa magonjwa katika sehemu hiyo.
Matumizi sahihi ya vifaa vya Electroniki; Mfano uwepo wa mitambo ya kuchakata na kutengeneza bidhaa.
Mahitaji ya wananchi; Mfano uwepo wa ajira mbalimbali katika kiwanda ili waweze kukidhi mahitaji yao.
Hivyo basi kiwanda kinatakiwa kuwa na mambo muhimu ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi;


Kielelezo Na.21: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 21, mtahiniwa alipata alama hafifu kwa kuwa hoja zake nyingi zinahusu mambo ya kuzingatia wakati kiwanda tayari kipo, isipokuwa hoja yake ya kwanza kuhusu eneo la ujenzi. Aidha, pamoja na kwamba kuzingatia afya za wananchi, usafi wa mazingira na matumizi sahihi ya vifaa ni mambo muhimu kuzingatiwa na viwanda, lakini hayana uzito ule ule kama vile uwepo wa mtaji, upatikanaji wa malighafi, uwepo wa nishati ya kutosha kuendesha kiwanda na uwepo wa wafanyakazi wenye ujuzi mambo ambayo yakikosekana kiwanda hakiwezi kuanzishwa na hata kikianzishwa itakuwa vigumu kukiendesha. Kwa hiyo, mambo aliyobainisha mtahiniwa ni muhimu wakati tayari kiwanda kipo.

### 2.2.2 Swali la: 12. Sayari Dunia

Swali la 12 lilitungwa kutoka mada ya Sayari Dunia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuchambua sababu tano zinazoweza kusababisha kutokea kwa majanga ya kibinadamu. Swali lilijibiwa na watahiniwa 854 sawa na asilimia 29.0 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili


ulikuwa mzuri kwani asilimia 98.8 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15. kama Chati Na. 12 inavyoonesha.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12.*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliofanya swali hilo, asilimia 64.3 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10, asilimia 34.5 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14.5 na watahiniwa wachache (1.7%) walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 34.5 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutoa hoja ambazo zilieleza sababu tano zinazoweza kusababisha kutokea kwa majanga ya kibinadamu. Sababu hizi ni kama vile, *uzembe katika uendeshaji wa vyombo vya usafirishaji vinavyoweza kusababisha ajali na kupoteza maisha ya watu wengi, uchafu uliokithiri unaoweza kusababisha mlipuko wa magonjwa kama vile kipindupindu, Uchafuzi wa mazingira unaoweza kusababisha milipuko ya magonjwa, uharibifu wa mazingira hasa ukataji miti ovyo ambao baadaye husababisha ukame na hatimaye kusababisha baa la njaa*. Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa walikuwa wana uwezo wa kutofautisha majanga ya kibinadamu na majanga ya asili; suala lililowafanya wajikite katika kutoa hoja zinazolingana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 22 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.



12. Majanga: Ni jumla ya mambo yote ambayo yana
tokea kwenye jamii au eneo flani na kupelekea Madhara
kwa majanga ya Asili na yale yasiyo ya Asili Mfano
wa Majanga: Mafuriko, Mlipuko wa Magonjwa, tetemeko
la Ardhi, Sunami, Ukame.
Sababu ambazo zinaweza kutokea kwa majanga
ya binadamu:
Uchafuzi wa mazingira/utupaji wa taka ovyo;
Uchafuzi wa mazingira huweza kutokea katika eneo
flani na kusababisha Majanga kwa binadamu mfano;
Janga la Mlipuko wa magonjwa mfano; Kipindupindu;
Kujenga nyumba katika mabonde: Chanzo kingine
cha kuweza kusababisha majanga ni kujenga nyumba
Sehemu ya mabonde ambapo Mvua ikinyesha hutoke
a Mafuriko ambayo ni moja ya Janga linaloleta
Madhara kwa mwanadamu.
Kukosa Elimu kuhusu majanga mbalimbali;
Majanga yanatokea kutokana na Wananchi kukosa
elimu kuhusu majanga namna yanavyoathiri
watu/binadam Mfano: Jamii kujenga kwenye
Mabonde hukosa Elimu mwisho ujikuta wanapa-
ta Madhara: Icho ni chanzo kikubwa cha Majanga
Kwa binadamu.
Ukame: Kutokana na ukame binadamu ana
weza pata Janga la njaa (ukosefu wa chakula).
hivyo basi ni vema kabla ya kuweka makazi
Sehemu kuzingatiu na Mazingira. Ukame ni janga
kubwa ambalo hepelekea watu kuwa wakimbizi
kutokana na Njaa inayotokana na Ukame.
Migogoro katika jamii: Ni chanzo cha
Majanga katika maisha ya binadamu kwamfano;

Kielelezo Na.22: Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 12.

Katika kielelezo Na. 21, mtahiniwa alitoa sababu tano zinazosababisha majanga ya kibinadamu kwa usahihi.

Katika swali hili, watahiniwa wengi (64.3%) walikuwa na ufaulu wa wastani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa watahiniwa hawa walikuwa wanaeleza shughuli mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha kutokea kwa majanga. Hata hivyo,

walishindwa kuthibitisha ni kwa namna gani shughuli hizo zinaweza kusababisha kutokea kwa majanga. Uchambuzi umebaini kuwa sababu za watahiniwa kushindwa kuthibitisha ilitokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya majanga. Ili tukio liwe janga, kuna mambo kadhaa inabidi yawe yametokea. Mambo hayo ni pamoja na jambo kutokea kwa ghafla na kuathiri watu wengi kwa mara moja. Kwa mfano, siyo kila ajali ni janga lakini ajali kama vile kuzama kwa meli (mfano Mv Bukoba) na ajali ya treni (kama vile ajali ya treni Dodoma) ni majanga kwa sababu yalihusisha watu wengi kwa mara moja kiasi cha kuhitaji timu za uokoaji kwenda kwenye eneo la tukio. Ingawa si kila ukame ni janga, lakini ukame unaosababisha watu wengi kukosa chakula na kusababisha watu hao kupoteza maisha na kuhitaji misaada ya dharura, ukame huo unakuwa ni janga. Kushindwa kwa watahiniwa kuweka muunganiko huo kwenye hoja zao kusababisha wengi wao kupata alama za wastani (6 – 10).

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (1.2%) waliokuwa na ufaulu hafifu walikuwa na changamoto ya kuchanganya dhana. Pamoja na kwamba mtahiniwa alitakiwa kueleza sababu za kutokea kwa majanga ya kibinadamu, wengi wa watahiniwa katika kundi hilo walichanganya matukio yanayosababisha majanga ya kibinadamu na matukio yanayosababisha majanga ya kiasili. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitoa hoja ambazo hazikuwa na ukweli kitaaluma, na hivyo kuwafanya wapate alama hafifu. Hoja hizo ni kama vile *uchimbaji wa madini ambao husababisha tetemeko la ardhi, ufugaji wa mifugo mingi ambao husababisha mmomonyoko wa udongo* na hoja kama vile, *kuanguka kwa vitu kutoka angani.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa sababu ingawa uchimbaji madini unaweza kusabbisha uharibifu wa mazingira, siyo kweli kwamba unasababisha kutokea kwa tetemeko la ardhi. Aidha, mmomonyoko wa udongo japo ni uharibifu wa mazingira haukidhi dhana ya janga kwa kuwa hutokea polepole. Ni kweli kuwa kuanguka kwa vitu kutoka angani kunaweza kuwa janga lakini si janga la kibinadamu bali ni janga la kiasili. Kielelezo Na. 23 ni sampuli ya majibu hafifu kutoka kwa mmojawapo wa watahiniwa katika kundi hili.

12 Majanga. Ni hali inayotokea kati
kati ya sura ya nchi ambayo inay
anawera kusababishwa na vitu
vya asili vilivyoko katika sura
ya nchi husika, mfano milima
mabonde, maji, bahari nk.

12 Zifuatazo ni sababu ambazo zin
aweza kusababisha kutokea kwa
majanga ya kibinadamu, nazo
ni kama zifuatazo.


Kukata miti ovyo; Husababisha
kutokea kwa janga la ukame
katika mazingira, hali hii husaba
bisha mazingira kuwa jangwa na
kukosekana kwa mvua za mara
kwa mara.

Kufuga mifugo mingi katika eneo
dogo, Hali hii husababisha kuto
kea kwa janga la tetemeko la
ardhi; ambapo huweza kuathiri
shughuli pamoja na makazi ya
binadamu.

Kuanguka kwa vitu vizito
kutoka angani kuanza bahari mf
ano magimba, vimondo, ambavyo
husababisha Tsunami, ambayo hu
sababisha maji ya bahari kuja
juu hadi kuanza kingo zake
na kusababisha majanga ya
mafuriko.

Milipuko ya Volkano; Hali hii
husababisha kutokea kwa tetome
ko la ardhi. Pia huweza kusaba
bisha kuharibu makazi ya vi
viumbe hai na binadamu pamoja
na vyo.

Maporomoko ya mawe kutoka
kuanza milima, wakati wa mvua




12 Kunyesha husababisha mafuriko - kwa baadhi ya sehemu za ukanda wa uchini wa sura ya nchi mfano sehemu za jangwa. Shughuli za binadamu mfano - uchimbaji wa madini husababisha kutokea kwa mafuriko pamoja na mmomonyoko wa ardhi. Hivyo basi ili kuzuia majanga hayo yasitokee tena tunapaswa kupanda miti kwa wingi na kuepuka kukata sehemu ambazo kunatokea sana majanga hayo.

Kielelezo Na. 23: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la *12.*

Katika kielelezo Na. 23, mtahiniwa alishindwa kubainisha tofauti ya majanga ya kibinadamu na majanga ya kiasili. Hii ilisababisha mtahiniwa kuchanganya hoja za majanga ya kiasili na majanga ya kibinadamu katika kujibu swali.

### 2.2.3 Swali la 13: Ushirikiano wa Kimataifa

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa. Katika swali hilo mtahiniwa alitakiwa kutoa tathmini ya changamoto zinazoikabili Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa. Takwimu zinaonesha kuwa, swali hilo lilijibiwa na watahiniwa 2,011 sawa na asilimia 68.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 90.1 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa muhtasari.




**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13.*

Kama Chati Na 13 inavyoonesha, kati ya watahiniwa waliofanya swali hilo, asilimia 20.0 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14, asilimia 70.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10 na asilimia 9.9 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri umenesha kuwa, watahiniwa hao waliweza kueleza changamoto zinazoikumba Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kiwango kinachoridhisha. Wengi wa watahiniwa hao walitoa hoja kama vile, *ukosefu wa fedha unaochangiwa na baadhi ya nchi wanachama kushindwa kutoa michango ya kuendesha jumuiya*. Watahiniwa pia walieleza uwepo wa ukosefu wa utulivu kama vile vitendo vya kigaidi katika baadhi ya nchi pamoja na migogoro katika baadhi ya nchi wanachama.

Hata hivyo, watahiniwa wengi walishindwa kuzibainisha changamoto za kimajukumu ya jumuiya kama vile; *kushindwa kuziunganisha nchi hizo na kuwa nchi moja; kushindwa mpaka sasa kuwa na sarafu moja itakayorahisisha shughuli za kibiashara katika jumuiya na kutokuwepo kwa jeshi la pamoja ili kuimarisha ulinzi katika jumuiya*. Kielelezo Na. 24 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua changamoto hizo kwa kiwango kizuri.

13. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)


Ni jumuiya inayounda nchi zilizopo mashariki mwa Afrika kama vile Kenya, Uganda, Tanzania. Jumuiya mpya ya afrika iliundwa mwaka 2002 ambapo ilikuwa na nchi tatu ambazo ni Kenya, Uganda na Tanzania. Mwaka 2007 nchi ya Rwanda na Burundi zilijiunga na Jumuiya hii. Na mwaka 2016 nchi ya sudani kusini ilijiunga na jumuiya ya Afrika mashariki ambapo kwa sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki ina wanachama sita (nchi sita). Zifuatazo ni changamoto za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa.

Ukosefu wa fedha. Hii ni changamoto inayoikumba Jumuiya ya Afrika Mashariki. Fedha za kuendeshea Jumuiya hiyo ni changamoto kwa Jumuiya hii. Baadhi ya nchi wanachama wanakumbwa na wimbi la umaskini. Hivyo basi fedha zinakosekana kwa ajili ya kuendeshea jumuiya hiyo.

13. Uwepo wa magonjwa. Hii pia ni changamoto ambayo inakumba Jumuiya ya Afrika Mashariki mfano Kuwepo kwa Ugonjwa wa Korona kuliletea changamoto kwa Jumuiya na wanachama wake. Ambapo shughuli mbali mbali za uzalishaji zilisimama. Pia hata Usafirishaji na mipaka ilifungwa.

Kuwepo kwa migogoro ya kisiasa. Hii nayo ni changamoto katika Jumuiya ya Afrika mashariki mfano mgogoro wa kisiasa wa "Sudani Kusini" Upia mgogoro wa kisiasa wa Rwanda. Migogoro hii ambayo huhusisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika mashariki huwa ni changamoto kubwa.

Kutofautiana kwa thamani ya Fedha Utofauto wa thamani ya fedha kati ya nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pia ni changamoto ambayo huikabili Jumuiya hii. Huonekana thamani ya fedha ya nchi fulani mwanachama iko juu au chini kuliko thamani ya fedha za nchi zingine Mfano fedha ya Tanzania iko chini kithamani na fedha ya Kenya.



13. Uwepo wa magonjwa. Hii pia
ni changamoto ambayo inaikumba
Jumuiya ya Afrika Mashariki mfano
Kuwepo kwa Ugonjwa wa Korona na
kuleta changamoto kwa Jumuiya na
wanachama wake. Ambapo shughuli mbali
mbali za uzalishaji zilisimama. Pia hata
Usafirishaji na mipaka ilifungwa.
Kuwepo kwa migogoro ya kisiasa.
Hii nayo ni changamoto katika Jumuiya
ya Afrika mashariki mfano mgogoro
wa kisiasa wa "Sudani Kusini" Upia
mgogoro wa kisiasa wa Rwanda.
Migogoro hii ambapo huhusisha nchi
wanachama wa Jumuiya ya Afrika
mashariki huwa ni changamoto kubwa.
Kutofautiana kwa thamani ya fedha
Utofauti wa thamani ya fedha kati
ya nchi mwanachama wa Jumuiya ya
Afrika Mashariki pia ni changamoto
ambayo huikabili Jumuiya hii.
Huonekana thamani ya fedha ya nchi
fulani mwanachama iko juu au chini
kuliko thamani ya fedha za nchi zingine
Mfano fedha ya Tanzania iko chini
kithamani na fedha ya Kenya.
Jumuiya ya Afrika Mashariki
hukumbwa na changamoto hizo ambapo
hufanya ishindwe kuendelea na
kupiga hatua. Changamoto hizo zikiweza
kutatuliwa kutakuwa na maendeleo


Kielelezo.Na. 24 Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 70.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu changamoto zinazoikabili Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watahiniwa hao walio wengi walijikita katika kueleza changamoto za kinchi kama vile; *masuala ya rushwa, ubovu wa miundo mbinu, tofauti za kimaendeleo* na *tofauti za lugha*, badala ya kuzungumzia changamoto ambazo ni kazi za msingi zinazotakiwa

kufanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kazi hizi ni kama vile *kuwa na sarafu moja, kuunda nchi moja, kuwa na jeshi la pamoja* na mambo kama vile *uwasilishaji wa michango wa nchi wanachama,* pamoja na *utatuzi wa migogoro iliyopo katika baadhi ya nchi wanachama*. Baadhi ya watahiniwa pia waliweka hoja bila ufafanuzi unaoonesha ni kwa namna gani hoja anayoitoa ni changamoto kwa jumuiya.

Upande wa asilimia 9.9 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu unaonesha kuwa hawakuwa makini katika kusoma swali na kulielewa. Jambo hilo lilidhihirishwa na watahiniwa hao kuandika majibu yaliyokuwa na maelezo ya kina lakini yasiyohusu mada iliyokuwa inatakiwa kujibiwa. Wengi wao walieleza faida zinazoweza kupatikana kwa nchi wanachama kuwa kwenye Jumuiya hiyo kama kielelezo Na. 25 kinavyoonesha.


13. Jumuiya afrika mashariki ni jumuiya
ambayo inaundwa na nchi mbalimbali za
Afrika mashariki ikiwemo Tanzania, kenya na
burundi kwa lengo la kutaka kuimarisha
mambo mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, ki
siasa na kiutamaduni Afrika mashariki.
Jumuiya ya Afrika mashariki inakumbwa na
changamoto mbalimbali ambazo zinaweza k
utatuliwa kwa namna mbalimbali.
Ifuatayo ni tathmini juu ya changamoto zin
azoikabili jumuiya ya Afrika mashariki:-
Kushirikiana katika kukuza na kui
marisha miundombinu mbalimbali miongoni
mwa nchi mwanachama, ili kuweza kusaidia
ka usafirishaji wa vitu mbalimbali na kuima
risha mawasiliano miongoni mwa nchi wanach
ama. mfano barabara na reli.
Kushirikiana katika kuimarisha ulinzi,
Umoja, amani na upendo miongoni mwa nchi
wanachama, ili kuwasaidia wanachama ku
endesha shughuli zao katika hali ya usalam
a pia kuepusha migogoro na vita ambavyo vi
nawoza vikatokea.



ka usafirishaji wa vitu mbalimbali na kuima
risha mawasiliano miongoni mwa nchi wanach
ama. mfano barabara na reli.
Kushirikiana katika kuimarisha ulinzi,
umoja, amani na upendo miongoni mwa nchi
wanachama, ili kuwasaidia wanachama ku
endesha shughuli zao katika hali ya usalam
a pia kuepusha migogoro na vita ambavyo vi
naweza vikatokea.
Kuimarisha shughuli za kiuchumi
miongoni mwa nchi wanachama, hii ita
saidia kukuza maendeleo ya nchi kiuchu
mi mfano kujenga viwanda mbalimbali
katika nchi wanachama.
Kuboresha huduma mbalimbali za kij
amii miongoni mwa nchi wanachama, ili ku
tatua changamoto za wanachama walizonazo
kwa kuwasogezea huduma mbalimbali karibu
18. mfano, huduma za Afya, umeme na elimu
ili kutatua changamoto hiyo miongoni mwa
nchi wanachama kwa wanachama wake.
Kudumisha na kuimarisha uhusiano
na ushirikiano mzuri miongoni mwa nchi
wanachama, nchi wanachama wanatakiwa
kushirikiana katika mambo mbalimbali
mfano, endapo nchi moja itakumbwa na janga
nchi wanachama wanapaswa kutoa misaada
mbalimbali kwa nchi hiyo.
Kwa ujumla, Jumuiya ya Afrika ma
shariki inakabiliwa na changamoto nyingi
hivyo inatakiwa kuwepo na misingi bora
itakayowaongoza katika shughuli zake na ku
weza kutatua changamoto zinazowakabili.


Kielelezo Na. 25: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13

Kama kielelezo Na. 25 kinavyoonesha, mtahiniwa alielekeza maelezo yake katika faida za nchi wanachama kuwa katika Jumuiya ya Afrika mashariki ambazo ni; *kushirikiana katika kukuza na kuimarisha miundombinu; kushirikiana katika kuimarisha ulinzi, umoja, amani na upendo; kuimarisha shughuli za kiuchumi, kuboresha huduma mbalimbali za kijamii na kudumisha na kuimarisha uhusiano na ushirikiano mzuri miongoni mwa nchi wanachama,* badala ya kujadili

changamoto zinazoikabili Jumuiya hiyo kama swali lilivyokuwa likimtaka mtahiniwa kujibu.

### 2.2.4 Swali la 14: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni. Katika swali hilo, watahiniwa walitakiwa kujadili sababu za mapambano ya Waafrika dhidi ya uvamizi wa kikoloni barani Afrika kuchukua sura tofauti. Swali hilo lilijibiwa na watahiniwa 937 sawa na asilimia 31.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Takwimu zinaonesha kuwa swali hilo ni kati ya maswali yenye ufaulu hafifu kwa kuwa ni asilimia 15.0 tu ya watahiniwa ndio waliokuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri kama Chati Na. 14 inavyoonesha.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14.*

Chati na 14 inaonesha kuwa asilimia 85.0 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5. Asilimia 11.8 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10, na asilimia 3.2 ndio pekee walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walitoa majibu ambayo hayakuwa na uhusiano na swali. Uchambuzi unaonesha kuwa, majibu ya baadhi ya watahiniwa yaliegemea katika kujadili hoja za mlengo uliotaka kujadili kwa nini waafrika walipinga uvamizi. Katika kujenga hoja zao katika mlengo huu watahiniwa walitoa hoja kama vile; *kupinga*

*kunyang'anywa aridhi, kupinga kulipa kodi katika serikali ya kikoloni* na *kupinga udhalilishwaji*. Watahiniwa wengine walieleza sababu za waafrika kushindwa katika mapambano ya kupinga uvamizi hasa pale walipotumia mapambano ya silaha. Watahiniwa walitumia hoja kama vile, *silaha duni zilizotumiwa na waafrika dhidi ya silaha za moto zilizotumiwa na wavamizi*; *kutokuwa na mbinu bora za kivita* na *kukosa ushirikiano miongoni mwa jamii za kiafrika*. Hoja kama hizi hazikujibu kiini cha swali ambacho kiliwataka watahiniwa kujadili ni kwa nini jamii za kiafrika zilipokea uvamizi wa kikoloni kwa sura tofauti. Watahiniwa katika swali hilo walitakiwa kujadili ni kwa nini baadhi ya jamii katika bara la Afrika hawakuupinga uvamizi huo kwa nguvu, na wengine waliupinga kwa nguvu na hata kutumia silaha. Kielelezo Na. 26 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambalo siyo sahihi.

14. Uvamizi wa kikoloni ni nama ya mataifa ya kikoloni kuingia nchi ~~ag~~ nyingine kimabavu kwa lengo la kunyonya uchumi wa nchi hiyo. Mapambano ya waafrika dhidi ya uvamizi wa kikoloni ulikuwa katika hatua mbili ambazo ni upinzani mdogo yaani hawakutumia nguvu nyingi Mfano walingo a mazao ~~yao~~ na upinzani mkubwa ambapo waafrika waliamua kutumia Mbinu za kivita ili kutoka mikononi wa wakoloni Mfano vita vya majimaji.

Yafuatayo ni sababu za kutokea kwa tofauti hizo kwa kutumia hoja mbalimbali kama vile;

Usaliti, usaliti wa baadhi ya viongozi ulichangia kwa kiasi kikubwa mapambano ya Afrika dhidi ya uvamizi wa kikoloni kwa sababu baadhi ya viongozi wa



14. Jadi walimatenga watu wao kwa kutoku-
kubali waafrika kupinga uvamizi wa
kikoloni.
Mtawanyiko wa familia, baadhi ya
familia zilitengana na hivyo kusababisha
watoto kusambaa mitaani bila sababu za
msingi zilizosababishwa na kutengana kwa
baadhi ya familia.
Maandalizi mabovu ya waafrika,
wakati wa vita waafrika walishindwa
kutokana na kutojiandaa kimapambano Mfano
kuchagua viongozi wakuu wa mapambano
na walitumia imani potofu.
Baa la njaa, waafrika walikumbwa na
baa la njaa kwa sababu wa mazao waliyo-
yapanda yaling'olewa na kuchomwa moto
mfano mazao ~~cha~~ yachakula kama mtama,
mahindi na karanga.
Silaha duni za waafrika, wakati
wa ~~ukoloni~~ mapambano ya waafrika
dhidi ya ~~ukolo~~ uvamizi wa kikoloni
waafrika hawakuwa na silaha bora za
kivitana kusababisha waafrika wengi
kuuawa Mfano wa silaha hizo ni kama
vile mikuki na pinde pia mapanga.
Hivyo basi ni vizuri kufanya
maandalizi mazuri kabla ya kwenda
kwenye mapambano ili kuonesha ushindi
na ushupavu wa wapambanaji.

Kielelezo Na. 26: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14.

Katika kielelezo Na. 26, hoja ya kwanza ilikuwa na ukweli ingawa wakati huo viongozi walioshirikiana na wavamizi hawakuwa na nia ya usaliti. Wakati ule, kila jamii ilijiona ni taifa tofauti kwa hiyo, ushirikiano wao na wavamizi ulilenga kupata washirika watakaowatumia kuwaangamiza wapinzani wao. Ushirikiano huo mara nyingi ulifanywa na jamii ambazo hazikuwa na nguvu kubwa za kijeshi ili kupata washirika wenye nguvu za kijeshi dhidi ya mahasimu wao. Kwa mfano, jamii ya Wasangu chini ya Chifu Melele dhidi ya Wahehe. Hata hivyo, hoja zilizofuata zilijikita katika kujadili sababu zilizosababisha waafrika kushindwa dhidi ya uvamizi wa kiloni kinyume na matakwa ya swali.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mchanganyiko wa hoja zinazoelezea sababu za Waafrika kushindwa vita wakati wa uvamizi wa kikoloni pamoja na hoja zilizoelezea sababu za Waafrika kupokea uvamizi wa kikoloni kwa namna tofauti. Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uwezo wa kupambanua bayana sababu zilizowafanya Waafrika kupokea uvamizi kwa namna tofauti, na sababu za Waafrika kushindwa vita dhidi ya mapambano wakati wa uvamizi. Watahiniwa hao waliyaona mambo hayo kama yanafanana.

Sababau ya watahiniwa wachache (3.2%) kuwa na ufaulu mzuri ni walielewa namna jamii za kiafrika zilivyopokea uvamizi wa kikoloni kwa namna ya kutofautiana. Uchambuzi ziadi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, baadhi yao walikuwa na mchanganyiko wa hoja. Hata hivyo, hoja nyingi zilijikita katika kuelezea namna jamii za Kiafrika zilivyopokea uvamizi wa kikoloni kwa namna inayotofautiana.


Sababu zilizotolewa na watahiniwa wengi katika kundi hili ni pamoja na; *tofauti za kimaendeleo, jamii zilizokuwa zimeendelea kiutawala na kijeshi ziliamua kupambana wakati jamii ambazo hazikuwa na maendeleo hayo zilishirikiana na wavamizi*. Hoja nyingine ni pamoja na matakwa binafsi ya viongozi. Viongozi hao kwenye baadhi ya jamii waliamua kupinga uvamizi huo wakati wengine waliwakaribisha. Hoja nyingine ni *uwepo wa wamisionari. Sehemu ambazo wamisionari walikuwa wameshaingia ziliwakaribisha wavamizi wakati jamii ambazo hazikuwa na wamisionari zilipinga*. *Uwepo wa majanga kama vile magonjwa* ni sababu pia iliyotolewa na watahiniwa katika kundi hili pamoja na *viongozi wa jamii husika kutojua nia ya ujio wa wakoloni*. Kielelezo Na. 27 ni sampuli ya majibu ya mojawapo wa watahiniwa waliojibu kwa kiwango kizuri.

19. la kuwanyonya Waafrika mali kuna sura tofauti tofauti ambazo zilitokea dhidi ya mapambano ya waafrika na uvamizi wa kikoloni, sababu ya tofauti hizo ni;-

Waafrika hawakujua lengo la wakoloni, Waafrika wengi hawakuweza kutambua sababu ya kuja kwa ukoloni na hiyo iliwapelekea waafrika kushindwa mapambano hayo. Mapambano hayo wakoloni walikuwa na lengo la kuchukua mali zao Waafrika lakini waafrika hawakuweza kutambua hilo.

Waafrika kutokuwa tayari kwa ajili ya mapambano, Waafrika walionekana kukosa utayari wa kupambania kwa masilahi yao hali hii iliwapelekea Waafrika kushindwa kwa Mapambano yao, kwa sababu walionesha kutokuwa na utayari wa kupambana.


Waafrika walikuwa wanategemea silaha kwa makoloni Hii iliweza kuwaletea sura tofauti ya kushindwa katika mapambano na kuweza kuwarudisha nyuma katika upambanaji wao, hiyo basi waafrika hawakujua sababu hiyo ya kuja kwa wakoloni nchini kwao kwa lengo na kwa namna ngani hawakuweza kupata nafasi zakushinda.


A. Viongozi wa kiafrika kuto-
kujua ujio wa wakoloni, Hii ili-
pelekea kuweza kuleta mapambano
na kushindwa kwa waafrika
kwa sababu hawakuwa na ufaha-
mu kuhusu ujio wao na malengo
yao ndani ya kwa kufanya
usuudi ngani katika kuendeleza
mikakati yao ya kikoloni.
Waafrika walizani watapata
utajiri kutoka kwa wakoloni, Hii
ilionesha kuwa kwa sababu hawa
kuwa na ufahamu wa kujua male-
ngo yao, hivyo waafrika walizani
ya kwamba endapo watakuweza
kushirikiana nao watapata utajiri
kutoka kwa wakoloni.
Kwa ujumla, Mapambano
ya Waafrika na wakoloni yalikuwa
ya namna mbalimbali na kuone-
sha sura mbalimbali, hivyo kulisa-
babisha ~~kuto~~ kuweza kuleta ma-
pambano ili kila taifa liweze
kulinda heshima yake hivyo
ili liweza kusababisha sura amba-
zo zilikuwa na namba mbalimbali.

Kielelezo Na.27: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14

### 2.2.5 Swali la 15: Upimaji na Tathmini

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Upimaji na Tathmini. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza namna tano ambavyo mwalimu anaweza kutumia kumbukumbu za upimaji endelevu katika kuboresha ufundishaji katika somo lake. Swali hilo lilijibiwa na watahiniwa wote 2,947. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hilo ulikuwa mzuri kwani asilimia 88.3 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa muhtasari.




**Chati Na. 15**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 15*

Kama Chati Na. 15 inavyoonekana, asilimia 27.0 ya watahiniwa waliofanya swali hilo, walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14. Asilimia 61.3 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10. Ni asilimia 11.7 tu ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kujibu swali hilo kwa usahihi. Waliweza kueleza namna mbavyo wanaweza kutumia kumbukumbu za upimaji endelevu katika kuboresha ufundishaji wa somo. Watahiniwa hao walitoa hoja ambazo zilienddana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuwa, *kumbukumbu za upimaji zanaweza kumsaidia mwalimu kufanya marekebisho ya zana za kufundishia ili kuwafanya wanafunzi waelewe dhana anazofundisha*. Watahiniwa pia walitoa hoja kuwa utunzaji wa kumbukumbu unaweza kumsaidia mwalimu kuboresha ufundishaji. Hoja kama hizo zilionesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri kuhusu matumizi ya kumbukumbu za upimaji endelevu katika ufundishaji. Kielelezo Na 28 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi katika swali hilo.

use only


15 Upimaji ~~enteleu~~ endelevu, hii ni aina ya upimaji ambao hufanyika muda wote katika-mchakato wa ujifunzaji ndani na nje ya-darasa. Hoja zifuatazo ni namna ambavyo mwalimu wa somo la jiografia anaweza kutumia kumbu-kumbu za upimaji endelevu wa wanafunzi kati-ka kuboresha ufundishaji katika somo lake.

Kubadilisha mbinu za kufundishia na-kujifunzia, Mbinu ni taratibu anazotumia mwalimu ili aweze kufanikisha malengo aliyo kusudia, kutokana na kumbu kumbu za upimaji endelevu mwalimu. anatambua kama mbinu alio itumia kama inafaa au haifai kutokana na kufanikiwa au kuto fanikiwa kwa malengo mahususi.

Humsaidia mwalimu abaini matatizo ya wanafunzi na kutafuta njia za kumsaidia, kutoka-na fomu ya mwenendo na tabia ya mwanafunzi. ambayo ni moja ya zana za upimaji endelevu mwalimu huweza kuwasaidia wanafunzi kutatua matatizo. waliyo nayo ili mchakato wa ufundishaji na ujifu-nzaji uwe wa ufanisi zaidi.

Kujua wanafunzi wenye mahitaji maalumu, baada ya kujua wanafunzi wanao hitaji msaada mwalimu anaweza kuboresha ufundishaji kwa ku-wasaidia ili wasijione wako tofauti na wanafunzi wengine ndani na nje ya darasa.

Upimaji endelevu utamjengea mwalimu uhu-siano mzuri kati yake mwanafunzi na mzazi au-mlezi, kunapo kua na uhusiano mzuri baina ya-mwalimu, mwanafunzi na mzazi husaidia kutatua-changamoto mbali mbali anazopitia mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, hali ambayo hupelekea-


15 Ufundishaji wa somo uwe wa ufanisi na mwa-
nafunzi anakua na uwezo wa kujifunza ~~kau~~ kwa
ari zaidi.
Upimaji endelevu hutumiwa na mwalimu ili-
kubadilisha zana za kufundishia na kujifunzia,
Zana ni kitu chochote anachotumia mwalimu ili-
kurahisisha ufundishaji wake. Pale mwalimu anapo
kua amewapima wanafunzi na lengo halijafanikiwa
mwalimu hupaswa abadilishe zana ili ~~ubo~~ ufundishaji
wake uwe bora zaidi.
Hivyo basi katika upimaji endelevu husi-
sisha katika masomo darasani. mwenendo wa-
mwanafunzi kitabia ndani na nje ya darasa
na upimaji huu upo kwa lengo la kuboresha -
ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na ~~wanafun~~
wanafunzi.


Kielelezo Na.28: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 15


Kama kielelezo Na. 28 kinavyoonesha, mtahiniwa alitoa hoja zilizojikita katika kuelezea namna ambavyo kumbukumbu za upimaji zinaweza kumsaidia mwalimu kuboresha ufundishaji wa somo la Jiografia, na hivyo kupata alama zilizomwezesha kuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo.

Kwa upande mwingine, asilimia 61.3 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walionesha uelewa wa wastani katika majibu yao. Watahiniwa hao, walikuwa na dosari kadhaa kwenye majibu yao kama vile, kurudia hoja kwa maneno mengine na wengine kutoa hoja ambazo hazikuwa zimejitosheleza katika kuelezea namna ambavyo mwalimu anaweza kutumia kumbukumbu za upimaji katika kuboresha ufundishaji.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu majibu walikuwa na majibu ya kina lakini, hayakuwa yameelekezwa katika kujibu hoja ya matumizi ya kumbukumbu za upimaji endelevu katika kuboresha ufundishaji. Baadhi ya watahiniwa walieleza namna ya kufanya upimaji badala ya matumizi ya kumbukumbu za upimaji endelevu. Wengine walieleza mambo yahusuyo upatikanaji wa zana za upimaji na zana za ufundishaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa, *upimaji endelevu unaweza kukafanyika kwa kutumia dodoso*

*hojaji, upimaji endelevu unaweza kufanyika kwa kutuia majaribio au kumaoezi darasasi.* Wengine pia walitoa hoja kama vile*; kutunza kubmukumbu za upimaji endelevu* lakini bila kutoa ufafanuzi. Kielelezo Na 29 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi.


15. Somo la jiografia, Ni somo ambalo linazungumzia binadamu na jumla ya vitu vinavyo mzunguka kwenye mazingira yake somo la jografia lina matawi ambayo ni kimaumbile, kwa vitendo na watu na uchumi jografia unaweza kufindisha kwa kutunzia kumbukumbu
Yafuatayo ni mambo ambayo mwalimu wa somo la jiografia anaweza kutumia katika kuboresha upimaji endelevu kwa kutunzia kumbukumbu za somo lake.
Kubandika, Mwalimu wa somo la jografia anaweza kutumia zana za upimaji endelevu kwa wanafunzi katika kuboresha ufundishaji katika somo lake kwa kubandika darasani.
Kuazima, Mwalimu wa somo anaweza kuboresha ufundishaji katika somo lake kwa kuazimisha mazana mbalimbali ili kuweze cha uboreshaji wake wa kile anachohitaji kufundisha kitunziwe kumbukumbu.
Kufaragua, Mwalimu wa somo anaweza kuboresha ufundishaji katika somo lake kwa kufaragua eneo ambalo wanafunzi ni rahisi kwao kupata na kuendelea kujifunza.
Kufinyanga, Mwalimu wa somo anaweza kuboresha ufundishaji kwa kufinyanga zana mbalimbali na wanafunzi na kisha wote kutenda kwa vitendo kulingana na madhumuni ya ufundishaji ili iweze kuwatunzia kumbukumbu za kudumu.




Chumba cha Kuifadhia zana, Mwalimu ana
weza kuboresha Upimaji endelevu kwa chumba cha
Kuifadhia zana, za Upimaji endelevu wakati
wa Ufundishaji kuchukuwa katika chumba
Mwalimu na kuanza kuzitumia.
Hitimisho, Mwalimu anapaswa kutumia zana
Kutunzia kumbukumbu kwa Upimaji endelevu
kwa kuazima, Chumba cha Kuifadhia zana,
Kuazima, Kufinyanga, Kufaragua, Kubandika
ili kuboresha Ufundishaji wake katika somo.

Kielelezo Na.29: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 15

Katika kielelezo Na. 29, mtahiniwa badala ya kueleza namna anavyoweza kutumia kumbukumbu za upimaji endelevu katika kuboresha ufundishaji, alieleza mambo yanayohusu matumizi ya zana, na namna mwalimu anavyoweza kupata zana za ufundishaji ambayo ni *kuazima, kufaragua,* na *kufinyanga*. Mtahiniwa pia alitoa hoja zinazohusu utunzaji wa zana alipoandika kuhusu *chumba cha kuhifadhia zana.*

### 2.2.6 Swali la.16. Ufundishaji wa Mada za Historia

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Historia. Katika swali hilo, watahiniwa walitakiwa kupendekeza mbinu tano zinazoweza kutumika katika kufundisha mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu. Swali hilo lilijibiwa na watahiniwa 2,945 sawa na asilimia 99.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Chati Na. 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa muhtasari.





**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 16*

Takwimu za ufaulu kama zinavyoonekana kwenye Chati Na. 16 zinaonesha kuwa, asilimia 71.6 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14.5. Asilimia 26. 0 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10 na asilimia 2.4 ndio pekee walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 61.2 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutoa mapendekezo sahihi ya njia nne hadi tano anazoweza kutumia mwalimu wa Historia kufundisha mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu na kutoa ufafanuzi sahihi. Watahiniwa hao walitoa njia mbalimbali kama vile *njia ya maswali dodoso*, *igizo dhima*, *hadithi*, *kualika mgeni mtaalamu wa eneo hilo* na *njia ya matembezi ya galari*. Watahiniwa hao pia walipendekeza njia nyingine kama vile *ziara mafunzo*, *majadiliano*, *kazi mafunzo* na *kazi mradi*. Mapendekezo hayo yalionesha kuwa watahiniwa walikuwa mahiri katika matumizi ya njia mbalimbali katika kufundisha mada hiyo. Kielelezo na 30 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyependekeza njia za ufundishaji wa mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu na kuzifafanua kwa usahihi.

16. Mabadiliko ya Binadamu; Mihatua alizopitia binadamu katika ukuaji-wake kuanzia hatua ya kwanza ambayo ni Australopithecus hadi hatua ya mwisho ambayo ni Homo Sapiens sapiens. Asili ya binadamu; ni dhimbuko la binadamu; zifuatazo ni njia anazoweza mwalimu kutumia katika kufundisha mada ya Asili na mabadiliko ya Binadamu.

Ziara mafunzo; Mwalimu anaweza kutumia njia ya ziara mafunzo katika kufundisha mada ya asili za binadamu kwa kuwachukua wanafunzi na kuwapeleka katika katika makumbusho-mbalimbali ya asili ya binadamu ili wawe kuelewa zaidi



Kazi mradi; Pia mwalimu anaweza kutumia njia ya kazi mradi katika kufundishia mada ya asili ya binadamu kwa kuwapa kazi wanafunzi ya kwenda kufanya utafiti kuhusiana na asili na mabadiliko ya binadamu katika makumbusho mbalimbali ya kihistoria.

Majadiliano; Mwalimu anaweza kutumia njia ya majadiliano ya makundi darasani kwa kutengeneza makundi mbalimbali na kuwaambia wajadiliane kuhusu asili na mabadiliko ya binadamu kulingana na wanavyoelewa wao. Hivyo itamsaidia mwalimu katika kufundisha.

16. Maswali na majibu; Hii ni mbinu-shirikishi ambayo mwalimu anaweza kutumia katika kufundishia mada ya Asili na mabadiliko ya binadamu kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali yanayohusu asili na mabadiliko ya binadamu na wao kuweza kujibu kulingana na uelewa wao.

Kualika mgeni; Pia mwalimu anaweza kutumia mbinu au njia ya kualika mgeni ambapo, mgeni huyo atakuwa na utaalamu zaidi au maarifa zaidi kuhusiana na asili na mabadiliko ya binadamu, hivyo na kuweza kuwaelezea wanafunzi kuhusiana na mada hiyo ya asili na mabadiliko ya binadamu.

Hivyo basi inashauriwa kwa mwalimu kutumia njia shirikishi zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wake.

Kielelezo Na.30: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 16

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu umeonesha kuwa, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia mbalimbali za kufundishia. Watahiniwa hao walipendekeza njia ambazo siyo rasmi; njia ambazo hazipo kwenye rejea mbalimbali za njia za ufundishaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza njia

kama vile, *njia ya maelekezo kutoka katika kitabu cha kiada, na njia ya nukuu rekodi.* Majibu kama haya yalionesha kuwa watahiniwa walikuwa wanabuni njia hizo. Walieleza mambo ambayo hayakutakiwa na swali kama vile hatua za mabadiliko ya binadamu kama yalivyoelezwa na mtaalam Charles Darwin; ambazo kimsingi siyo njia za kufundishia. Kielelzo Na. 31 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambalo halikuwa sahihi.

16 Asili ya mabadiliko ya binadamu ni zile hatua zote ambazo binadamu ali pitia; kama vile Australopithecus, ikiwaka ma hatua ya kwanza kabisa ya mfumo wa maisha ya binadamu.


Unaweza kutumia njia ya kuwaeleza w ana funzi hatua tano za asili ya ma badiliko ya binadamu kama ifuatavyo.

Australopithecus; katika hatua hii unawaeleza wanafunzi kuwa bina damu wa kwanza alitokana na nyani m wenye jamii ya sokwe mtu, ambaye ali ishi porini akiwa na manyoya na pia alitembea kwa miguu minne.

Zinjan thropus; Hii ni hatua ya pili ya mabadiliko ambapo sokwe huyo aliweza kula matunda ya porini na kuchimba mizizi aliyoitumia kama chakula chake.

Homo habilis; Hii ni hatua ya ta tu ambapo sokwe huyo alianza kupu ngua manyoya... ambapo alianza kuinuk a juu miguu yake ya mbele kutokana na kurukia matunda.

Homo erectus; katika hatua hii binadamu alinyanyuka kabisa kwa sababu ya kutamani matunda yali yo juu ya miti mirefu hivyo aliwez a kuyachuma bila shida na uwezo wake wa akili ukaongezeka.



16. Homo Sapiens; Katika hatua hii binadamu aliweza kutembea kwa miguu miwili na kushika silaha kwa miguu ya mbele ambayo kwa sasa ni mikono. Uwezo wake wa akili uliongezeka pia aliweza kuwinda, kutumia moto na kujikinga na wanyama wakali.

Ufundishaji unaozingatia mahitaji ya zana ni muhimu sana kwa mwalimu ili kuweza kufundisha kwa ufanisi. Hivyo mwalimu anapofundisha kila hatua azingatie mahitaji ya zana kwa wanafunzi ili waweze kumuelewa kwa ufasaha.

Kielelezo Na. 31: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 16

Kama kielelezo Na. 31 kinavyoonesha, katika mapendekezo yake, mtahiniwa alipendekeza kuwa atatumia njia ya kuwaeleza wanafunzi mabadiliko ya binadamu na kuanza kueleza hatua ambazo binadamu alipitia kwa mujibu wa Darwin. Hata kama tutachukulia kuwa neno kuwaeleza lilimaanisha kutumia njia ya mhadhara, inamanisha kuwa mtahiniwa alipendekeza njia moja tu ya kufundishia badala ya tano alizotakiwa kupendekeza.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali za mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa mzuri. Kati ya mada 10 zilizotahiniwa, ufaulu ulikuwa mzuri katika mada tano, wa wastani katika mada nne na hafifu katika mada moja. Mada zilizokuwa na ufaulu mzuri ni *Upimaji na Tathmini (98.3%)*, *Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo (97.6%)*, *Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira* (97.3%), *Ushirikiano wa Kimataifa (90.1%),* na *Nchi Yetu Tanzania (88.4%).* Mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani ni pamoja na *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika (64.9%), Sayari Dunia (62.6%), Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika (53.8%)* na mada ya *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa, Kiuchumi katika Afrika Huru (49.0). mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani* ilikuwa na ufaulu hafifu wa asilimia 37.0.

Uchambuzi Zaidi ulifanyika ili kubaini mwenendo wa ufaulu katika mada hizo kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2019 hadi 2021. Uchambuzi huo umebaini kuwa, ufaulu umeendelea kuwa mzuri katika mada tano, za *Upimaji na Tathmini, Nchi YetuTanzania, Ushirikiano wa Kimataifa, Asili na Mabadiliko ya Binadamu Technolojia na Mazingira,* na *Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo.* Ufaulu umeshuka kutoka ufaulu mzuri hadi kuwa wa wastani katika mada mbili za *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika, Sayari Dunia* na *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru.* Ufaulu umeendelea kuwa wa wastani katika mada moja ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni*. Mada moja ya *Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani* ufaulu wake umeshuka kutoka mzuri hadi hafifu. Aidha, mada moja ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika* imeendelea kuwa na ufaulu wa wastani kwa miaka yote mitatu.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa taarifa hii umeonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ni mzuri. Hata hivyo, ikilinganishwa na ufaulu katika somo hilo mwaka 2020, ufaulu umeshuka katika baadhi ya mada. Uchambuzi umeonesha ongezeko la mada zenye ufaulu wa wastani kutoka moja mwaka 2020 mpaka mada nne katika mwaka 2021. Aidha, wakati mwaka 2020 hapakuwa na mada yenye ufaulu hafifu, mwaka 2021 kumekuwa na mada moja yenye ufaulu hafifu. Kushuka kwa ufaulu katika mada hizo kumesababisha kushuka kwa ufaulu kwa ujumla katika matokeo ya watahiniwa ya mwaka 2021 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2020.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, ufaulu hafifu katika maswali ambayo watahiniwia walikuwa na ufaulu hafifu mara nyingi haukutokana na watahiniwa kutokuwa na maarifa kabisa; bali ulitokana na kutozingatia maelekezo ya maswali na hivyo watahiniwa hao walijikuta wanatoa majibu ya kina lakini ambayo hayaendani na swali waliloulizwa. Watahiniwa pia walibaika kuwa na changamoto ya kuchanganya dhana wakati wa kujibu maswali. Aidha, watahiniwa pia walikuwa wanashindwa kujenga hoja hasa katika maswali ya kujieleza zinazoendana na swali waliloulizwa. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, taarifa hii itasaidia wadau hasa wakufunzi na wanachuo katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika mada moja ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani ambayo

ilikuwa na ufaulu hafifu, na mada nne za Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru, Sayari Dunia, Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika, na Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika ambazo zilizokuwa na ufaulu wa wastani.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua ufaulu katika mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani, ambao ulikuwa wa kiwango hafifu na mada ya Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika ambayo imeendelea kuwa na ufaulu wa wastani, yafuatayo yanapendekezwa kufanyika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

(a) Katika kuimarisha ufaulu katika mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani;

(i) Wanachuo wajifunze kwa vitendo vipengele muhimu vya ramani yaani; kichwa cha habari cha ramani, ufunguo na kipimo cha ramani. Wanachuo washiriki katika kubuni kichwa cha habari cha ramani pamoja na kubainisha alama zinazotumika kwenye ramani na utambuzi wake zinapotumika kwenye ramani. Wanachuo pia washirikishwe katika matumizi ya kipimo cha ramani ambayo yameonekana kuwasumbua wataniwa wengi.

(ii) Wanachuo wapewe kazi mradi kuhusu uchoraji wa ramani zikilenga kuwasaidia wanachuo kuhusu matumizi ya vitu muhimu vinavyounda ramani ili kuwajengea uelewa wa usomaji wa ramani na namna kila kipengele cha ramani kinavyoweza kutumika.

(b) Katika kuinua ufaulu katika mada ya Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika;

(i) Wanachuo washirikishwe katika kujifunza mada hiyo kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile usomaji bainifu wa maandiko ili waweze kuwa na maarifa mapana kuhusu namna jamii mbalimbali zilivyopokea au kupambana na uvamizi wa kikoloni.

(ii) Njia za kuwashirikisha wanachuo kuongeza uelewa zitumike katika kujifunza mada hiyo kama vile kuwapa wanachuo kazi mradi ili waweze kutafuta taarifa kuhusu upinzani dhidi ya uvamizi wa kikoloni barani Afrika.

**KIAMBATISHO**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MTIAHNI WA MAARIFA YAJAMII

| Na. | Mada | Na. ya Swali | Ufaulu katika kila Swali (%) | Wastani wa ufaulu mmada | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | *Upimaji na Tathmini* | 15 | 98.3 | 98.3 | Vizuri |
| 2. | *Ufundishaji wa somo* | 16 | 97.6 | 97.6 | Vizuri |
| 3. | *Asili na mabadiliko ya Binadamu, TEknolojia na mazingira* | 7 | 97.3 | 97.3 | Vizuri |
| 4. | *Ushirikiano wa kimataifa* | 13 | 90.1 | 90.1 | Vizuri |
| 5. | *Nchi Yetu Tanzania* | 1 | 67.3 | 88.4 | vizuri |
| | | 11 | 99.3 | | |
| | | 12 | 98.8 | | |
| 6. | *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika.* | 6 | 64.9 | 64.9 | Wastani |
| 7. | *Sayari Dunia* | 2 | 20.3 | 62.6 | Wastani |
| | | 3 | 68.5 | | |
| | | 4 | 99,2 | | |
| 8. | *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika.* | 14 | 15.0 | 53.8 | Wastani |
| | | 10 | 92.6 | | |
| 9. | *Mabadiliko nya Kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru* | 8 | 13.6 | 49 | Wastani |
| | | 9 | 84.4 | | |
| 10. | *Stadi sahili na tata za picha na Ramani* | 5 | 37.0 | 37.0 | Hafifu |